**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

# TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2023 HADI JANUARI, 2024 PAMOJA NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA, JULAI HADI DESEMBA, 2023

*[Inatolewa chini ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

Ofisi ya Bunge,

10 Barabara ya Morogoro,

S.L.P. 941,

41105 Tambukareli,

**DODOMA**

14 Februari, 2024

## YALIYOMO


**SEHEMU YA KWANZA ........................................................................ 1**

**1.0. UTANGULIZI ........................................................................ 1**

1.1. Muundo wa Taarifa ........................................................................ 1

1.2. Majukumu ya Kamati ........................................................................ 1

1.3. Majukumu yaliyotekelezwa na Kamati ........................................................................ 2

**SEHEMU YA PILI ........................................................................ 4**

**2.0. MASUALA YALIYOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI ........................................................................ 4**

2.1. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23 ........................................................................ 5

2.1.1. Viashiria vya Uchumi Jumla ........................................................................ 5

2.1.2. Mwenendo wa Mapato na Matumizi ........................................................................ 10

2.1.3. Masuala yaliyobainika kwenye Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/23 ........................................................................ 13

2.1.3.1. Maombi ya Fedha nje ya Fungu ........................................................................ 13

2.1.3.2. Miradi ya Maendeleo kutokamilika kwa Wakati ........................................................................ 13

2.1.3.3. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ........................................................................ 14

2.1.4. Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023 .... 15

2.2. Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023 (The Finance Bill, 2023) ........................................................................ 16

2.3. Tathmini ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/25 pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 ........................................................................ 17

2.3.1. Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Utekelezaji wa Mpango ........................................................................ 18

2.3.2. Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi za Umma Kutoshirikiana wakati wa Kupanga na Kutekeleza Miradi ........................................................................ 18

2.3.3. Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti ........................................................................ 19

2.4. Hoja Mahsusi ........................................................................ 20

**2.4.1. Hoja zilizotokana na Kamati za Bunge za Kisekta (Kanuni ya 117)** ........................................................................ 20

2.4.2. Hoja zilizotokana na Mjadala Bungeni wakati wa Kujadili Bajeti za Wizara (Kanuni ya 124) 20

2.5. Ziara za Kamati za Kukagua Miradi ya Maendeleo pamoja na mafunzo ........................................................................ 27

2.5.1. Masuala muhimu yaliyojitokeza ........................................................................ 28

2.5.1.1. Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP) ........................................................................ 28

2.5.1.2. Miradi ya Ujenzi wa Mabwawa ya Umwagiliaji pamoja na Mashamba ya Mbegu..... 29
2.5.1.3. Mradi wa Maji wa Buzuruga ........ 30
2.5.1.4. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Kisasa ya Mwendokasi (SGR) ........ 31
2.6. Mafunzo kwa Kamati ........ 34
**SEHEMU YA TATU ........ 36**
**3.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KATIKA KIPINDI CHA NUSU MWAKA (TAREHE 1 JULAI HADI TAREHE 31 DESEMBA 2023) ........ 36**
3.1. VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA ........ 37
3.1.1. Ukuaji wa Uchumi ........ 37
3.1.2. Akiba ya Fedha za Kigeni ........ 38
3.1.3. Mfumuko wa Bei ........ 38
3.1.4. Mikopo Chechefu ........ 39
3.1.5. Mikopo kwa Sekta Binafsi ........ 39
3.1.6. Ujazi wa Fedha ........ 41
3.1.7. Thamani ya Shilingi ........ 42
3.1.8. Mwenendo wa Viwango vya Riba ........ 42
3.1.9. Thamani ya Bidhaa na Huduma ........ 43
3.1.10. Deni la Serikali ........ 44
3.2. Mwenendo wa Mapato na Matumizi ........ 46
3.2.1. Mwenendo wa Mapato hadi Desemba, 2023 ........ 46
3.2.1.1. Mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ........ 46
3.2.1.2. Mapato yasiyo ya Kodi ........ 47
3.2.1.3. Mikopo na Misaada Nafuu ........ 49
3.2.2. Mwenendo wa Matumizi hadi Desemba, 2023 ........ 50
3.3. Malimbikizo ya Madeni (Arrears) ........ 51
**SEHEMU YA NNE ........ 53**
**4.0. TATHIMINI YA UTEKELEZAJI WA MABORESHO YA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2023 PAMOJA NA MABADILIKO YA SHERIA YA USHURU WA FORODHA YA AFRIKA MASHARIKI YA MWAKA 2004 ........ 53**
4.1. Tathmini ya Utekelezaji wa Baadhi ya Sheria zilizokuwa kwenye Sheria ya Fedha ........ 54

4.1.1. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 ... 54
4.1.2. Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82. ... 55
4.1.3. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 ... 55
4.1.4. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 ... 55
4.1.5. Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Sura ya 437 ... 56
4.1.6. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 ... 56
4.1.7. Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004 (EAC Custom Management Act, 2004) ... 56
4.2. Mapendekezo ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Sheria ya Fedha. ... 57
**SEHEMU YA TANO ... 58**
**5.0. MWELEKEO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA NA BAJETI YA SERIKALI HADI JUNI, 2024 ... 58**
5.1. Malengo na Shabaha ... 58
5.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Januari – Juni, 2024 ... 60
**SEHEMU YA SITA ... 61**
**6.0. UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YALIYOTOKANA NA TAARIFA YA KAMATI YA MWAKA 2023 ... 61**
6.1. Tathmini ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ... 62
6.1.1. Maazimio yaliyofanyiwa Kazi na Serikali ... 62
6.1.1.1. Kurejesha Tume ya Taifa ya Mipango ... 62
6.1.1.2. Mtaji kwa Kampuni ya Taifa ya Mbolea – TFC ... 62
6.1.1.3. Mifumo ya TEHAMA ya kukusanya mapato kutosomana ... 63
6.1.1.4. Usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Serikali ... 64
6.1.1.5. Mkopo wa asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ... 64
6.1.2. Maazimio ambayo yapo katika hatua za utekelezaji ... 65
6.1.2.1. Mpango wa Uhitaji wa Rasilimali watu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi ... 65
6.1.3. Maazimio ambayo hayajafanyiwa kazi ... 65
6.1.3.1. Kuanzisha Mfuko wa Dharura (Contingecy Fund) ... 65
6.1.3.2. Nyongeza ya fedha kwa Shirika la Hifadhi la Taifa – TANAPA ... 66
6.1.3.3. Kuongeza jumla ya shilingi bilioni 45.56 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya kipaumbele ya Sekta ya Anga ... 66
6.1.3.4. Vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kupewa kipaumbele katika mradi wa Kujenga Kesho iliyo Bora (BBT) pamoja na ajira zinazotolewa na Kampuni Tanzu ya SUMA (JKT) 66

**SEHEMU YA SABA** ........................................................................................ **66**

**7.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA UJUMLA** ............................................ **66**

7.1. Mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa ........................................ 66
7.2. Masoko ya Kikanda (Regional Integration) ................................................... 67
7.3. Viwango vya Riba kwenye Mabenki kwa Watumishi wa Umma ..................... 68
7.4. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kushiriki katika uwekezaji wa Hatifungani ......... 68
7.5. Utolewaji wa Fedha katika Mafungu Mbalimbali ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 69

**SEHEMU YA NANE** ........................................................................................ **69**

**8.0. MAONI NA MAPENDEKEZO MAHUSUSI** ............................................ **69**

8.1. Matumizi ya Seti ya Mitambo ya kuchimba visima na mabwawa ..................... 69
8.2. Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Fedha Haramu ........................................... 70
8.3. Utekelezaji wa miradi ya barabara kwa Mfumo wa Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ........................................................................................ 71
8.4. Serikali iandae Sera na mkakati wa Ununuzi, Ugavi na uondoshaji Mali za Umma ......... 71
8.5. Fedha za Mkopo wa ECF kujumuisha Sekta ya Utalii ....................................... 72
8.6. Uwepo wa Sera na Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini ........................................ 72
8.7. Kutungwa kwa Sheria na Sera ya Usimamizi wa Mali za Serikali (*Government Assets Management Division*) ........................................................................................ 73
8.8. Riba za Mikopo katika Sekta ya Benki ............................................................ 73
8.9. Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Miradi ya Maendeleo ............... 74

**SEHEMU YA TISA** ........................................................................................ **76**

**9.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO** ........................................................ **76**

9.1. Mafanikio katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati .................................... 76
9.2. Changamoto katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati ................................ 77
9.2.1. Ucheleweshwaji wa Taarifa kutoka Serikalini ................................................ 77
9.2.2. Tofauti ya Takwimu baina ya Wizara na Taasisi za Serikali kuhusiana na jambo moja ...... 78
9.2.3. Kukosekana kwa utaratibu maalumu wa kikanuni wa kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ..................................................... 78

**SEHEMU YA KUMI** ........................................................................................ **80**

**10.0. HITIMISHO** ........................................................................................ **80**

**KIAMBATISHO A.** ........................................................................................ **82**

**KIAMBATISHO B. .................................................................................................. 83**

**KIAMBATISHO C. .................................................................................................. 86**

# TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2023 HADI JANUARI, 2024 PAMOJA NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA, JULAI HADI DESEMBA, 2023

*[Inatolewa chini ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

## SEHEMU YA KWANZA
## MAELEZO YA JUMLA

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa majukumu katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024, pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka Julai hadi Desemba, 2023 na mwelekeo hadi Juni, 2024.

### 1.1. Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu kumi kama ifuatavyo; Sehemu ya kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili ni Masuala yaliyobainika katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati, Sehemu ya Tatu ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Katika Kipindi cha Nusu Mwaka, Sehemu ya Nne ni Utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2023, Sehemu ya Tano ni Mwelekeo wa Viashiria vya Uchumi Jumla na Bajeti ya Serikali hadi Juni, 2024, Sehemu ya Sita ni Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya ya Mwaka 2023 ya Kamati ya Bajeti, Sehemu ya Saba ni Maoni na Mapendekezo ya Ujumla, Sehemu ya Nane ni Maoni na Mapendekezo Mahsusi na Sehemu ya Tisa ni Mafanikio na Changamoto na Sehemu ya Kumi ni Hitimisho.

### 1.2. Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa masharti ya Kifungu

cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 pamoja na Nyongeza ya Nane, Fasili ya 9, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi Kamati ilitumia nyaraka mbalimbali kama vile Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2021/22 na 2022/23, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 hadi 2025/26, Mpango wa Taifa wa Mwaka 2021/22 na 2022/23, machapisho mbalimbali ya Taasisi za ndani na Kimataifa kama vile Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (WB), Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na tafiti mbalimbali zilizofanywa na Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

### 1.3. Majukumu yaliyotekelezwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilitekeleza majukumu yafuatayo: -

a) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23;
b) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa nusu mwaka 2023/24;
c) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 na robo ya kwanza ya mwaka 2023/24;
d) Kuchambua na kujadili Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24;
e) Kuchambua na kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na mafungu nane yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2022/23;
f) Kuchambua na kujadili makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha pamoja na Mafungu nane yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2023/24;

g) Kuchambua na kujadili utekelezaji wa Bajeti za Mifuko ya Mahakama, Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23, pamoja na kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Mifuko hiyo kwa Mwaka wa fedha 2023/24;
h) Kuchambua na kushauri kuhusu mapendekezo ya mabadiliko ya sheria mbalimbali kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023 (The Finance Bill, 2023);
i) Kujadili na kutoa maoni kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi SURA 103;
j) Kujadili na kutoa maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023;
k) Kuchambua na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/25;
l) Kuchambua Taarifa za utekelezaji wa Bajeti na Utendaji kazi wa Wizara ya Fedha pamoja na Idara, Taasisi, Wakala na Mamlaka mbalimbali zilizo chini yake;
m) Kuchambua Taarifa ya utendaji kazi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2022/23;
n) Kushiriki mafunzo mbalimbali yenye lengo la kuwaongezea uwezo Wajumbe wa Kamati katika nyanja za kodi, fedha, uchumi, uwekezaji, ujenzi wa miundombinu pamoja na mifumo mbalimbali ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato;
o) Kukutana na wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi ili kupokea maoni, mapendekezo na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria za kodi na zinazosimamia biashara na uwekezaji zinazoathiri Sekta binafsi. Baadhi ya Wadau waliofika mbele ya Kamati ni wafuatao: - Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Jumuiya ya Wazalishaji Viwandani (CTI), Chama cha Wazalishaji wa Chumvi (TASPA), Chama cha Mabenki Tanzania (TBA), Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini Tanzania (FEMATA), Kampuni ya Saruji ya Mbeya, Kampuni ya Bia ya Tanzania (TBL) na Kampuni ya Bia Serengeti (SBL), Kampuni ya Asas Dairies Ltd, Kampuni ya Madini ya Barrick, Shirikisho la Wachimba Madini (Tanzania Chamber of Mines), Kampuni

ya Sigara (TCC), Kampuni ya Ferrotch Africa Ltd, Jumuiya ya Kampuni za Uwindaji wa Kitalii Tanzania (TAHOA), Tanzania Association of Tour Operators (TATO), Chama Cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Tanzania Air Operators, Chama cha Wachezeshaji Michezo ya Kubahatisha (TSBA), Taasisi ya Wafanyabiashara wa Mafuta rejareja Tanzania (TAPSOA), Baraza la Kilimo Tanzania (ACT), Chama cha Wamiliki wa Malori (TATOA), Chama cha Waagizaji na Wasambazaji wa Mafuta Tanzania (TAOMAC), Umoja wa Makampuni ya Simu Tanzania (TAMNOA), Research on Poverty Alleviation (REPOA), Taasisi ya Wajibu, ESRF pamoja Taasisi ya GATSBY;

p) Kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato na kutoa mapendekezo kuhusu vyanzo vipya vya mapato ili kupunguza utegemezi wa kibajeti;
q) Kuchambua na kujadili Hoja Mahsusi kwa mujibu wa Kanuni ya 117 na 124 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Tolea la Februari, 2023;
r) Kutembelea na kukagua utekelezaji wa mradi wa Kimkakati wa Kufua Umeme wa Mwalimu Nyerere (JNHPP), miradi ya maendeleo ya ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ya Chinangali na Mwembe (Dodoma), Tlawi (Manyara), Mashamba ya TARI na ASA (Arusha), Msingi (Singida), Tabora na Mkombozi (Iringa); na
s) Kutembelea Taasisi mbalimbali ili kukagua utendaji kazi wake. Taasisi zilizotembelewa ni OSHA, NIDA, BPA, TPA na PPRA, TAEC.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0. MASUALA YALIYOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilibaini masuala yafuatayo: -

## 2.1. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23

### 2.1.1. Viashiria vya Uchumi Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 kwa kuangalia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi jumla na kutoa ushauri kama ifuatavyo: -

**a) Pato la Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2022 Pato la Taifa lilikua kwa **asilimia 4.7** ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 4.9** mwaka 2021. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na athari ya vita kati ya Urusi na Ukraine iliyosababisha kupanda kwa gharama za uzalishaji katika baadhi ya sekta, mabadiliko ya tabianchi yaliyoathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa baadhi ya maeneo nchini na kudorora kwa uchumi wa dunia kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kiwango hicho cha ukuaji kilitokana na mikakati mbalimbali iliyochukuliwa na Serikali kukabiliana na athari za vita nchini Ukraine, uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan makaa ya mawe, jasi, chumvi, almasi, mawe ya chokaa na shaba na kuongezeka kwa shughuli za utalii. Kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia iliyotolewa tarehe 01 Julai 2023, Tanzania imeendelea kubaki kuwa miongoni mwa nchi zenye uchumi wa kipato cha chini cha kati ambapo wastani wa pato kwa kila mtu (GNI Per Capita) limeongezeka kutoka **dola ya Marekani 1,140** mwaka 2021 hadi **dola ya Marekani 1,200** mwaka 2022.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake katika kukuza uchumi, hata hivyo ina ushauri ufuataо:-

i. Kwa kuwa moja ya sababu iliyochangia kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi ni vita inayoendela kati ya nchi ya Urusi na Ukraine, vita hiyo inaweza kuwa fursa badala

ya kikwazo cha kiuchumi kwa kuangalia ni namna gani Serikali inaweza kuongeza uzalishaji mfano katika Mafuta ya kula kwa ajili ya kuuza nje ya nchi, matumizi ya gesi asilia, uzalishaji wa mbolea, na kilimo cha ngano hasa kwenye mashamba makubwa kama vile ya Basotu.

ii. Katika kipindi cha miaka 2 sekta zinazokua kwa kasi na kuchangia katika uchumi ni zile ambazo ukuaji wake unachagizwa na uwekezaji wa Serikali isipokuwa sekta ya Sanaa na burudani. Sekta hizo ni Madini, Umeme, Fedha na Bima. Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa sekta ambazo zinaendeshwa na kusimamiwa na sekta binafsi kwa mfano uzalishaji viwandani, huduma, chakula na malazi, pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi iliyopo katika Sekta za Uvuvi, Kilimo na Mifugo ili kuchochea ukuaji wa sekta hizo. Hatua hizo zitawezesha kufikia malengo ya ukuaji wa uchumi kwa **asilimia 5.3** kwa mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 1 Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa, 2018 – 2023**




| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka | 7.0% | 7.0% | 4.8% | 4.9% | 4.7% | |
| Robo ya Kwanza | 7.4% | 6.3% | 5.3% | 5.0% | 5.5% | 5.6% |

***Chanzo**: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/23*

**b) Mfumuko wa Bei**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23 mfumuko wa bei uliongezeka kwa wastani wa **asilimia 4.6** ikilinganishwa na **asilimia 4.0** katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Mfumuko wa bei ulikuwa **asilimia 3.6** Juni, 2023 ikilinganishwa na **asilimia 4.4** katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa bei ya bidhaa na huduma zinazoagizwa kutoka nje ya nchi hususan bidhaa za petroli, mafuta ya kula, mbolea, ngano na malighafi za viwandani ambazo zilisababisha kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la ndani, kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya ndani kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kuongezeka kwa mahitaji ya chakula kutoka nchi jirani hususan ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia kutokana na athari za vita vinavyoendelea kati ya Ukraine na Urusi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto hizo mfumuko wa bei ulibaki ndani ya lengo la nchi la kati ya **asilimia 3** hadi **asilimia 7**, na vigezo vya mtangamano vya Jumuiya ya Afrika

Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika vya **asilimia 8.0** na kati ya **asilimia 3** hadi **asilimia 7**, mtawalia. Aidha, katika kapu la Bidhaa na Huduma, vyakula na vinywaji baridi vinabeba uzito wa **asilimia 28.2** ambao ni mkubwa kuliko bidhaa na huduma nyingine ikifuatiwa na makazi, maji, umeme, gesi, samani na matengenezo ya makazi **asilimia 15.1** pamoja na usafiri **asilimia 14.1** katika kapu hilo. Hivyo, endapo kutakuwa na upungufu wa chakula kutakuwa na uzito mkubwa katika kuchochea ongezeko la mfumuko wa bei.

**c) Mwenendo wa Thamani ya Shilingi**

**Mheshimiwa Spika,** thamani ya **shilingi ya Tanzania** imeendelea kuwa tulivu na thabiti ambapo katika mwaka 2022/23, **dola moja ya Marekani** ilibadilishwa kwa wastani wa **shilingi 2,334.30** ikilinganishwa na **shilingi 2,313.96** mwaka 2021/22, sawa na kushuka thamani (*depreciation*) kwa **asilimia 0.9**. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba kwa miaka mitatu mfululizo **Shilingi ya Tanzania** imeendelea kushuka thamani kwa kiwango kidogo ulikinganisha na sarafu za nchi zinazotuzunguka. Mfano, katika mwaka 2020/21, **dola moja ya Marekani** ilibadilishwa kwa wastani wa **shilingi 2,310.18**, na mwaka 2021/22 **dola moja ya Marekani** ilibadilishwa kwa wastani wa **shilingi 2,313.96** sawa na kushuka thamani kwa **asilimia 0.2**. Vilevile, katika mwaka 2022/23, **dola moja ya Marekani** ilibadilishwa kwa wastani wa **shilingi 2,334.30** sawa na kushuka thamani kwa **asilimia 0.9** ikilinganishwa na mwaka 2021/22**.**

**Mheshimiwa Spika,** kushuka kwa thamani ya shilingi kuna athari nyingi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa thamani ya deni la Serikali na bajeti Serikali ya kutekeleza miradi ya maendeleo inayotegemea uagizwaji wa vifaa kutoka nje ya nchi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya muda mfupi, kati na mrefu ya kukabiliana na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani, mfano kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje, kupunguza

uagizaji wa bidhaa kutoka nje zinazozalishwa nchini na kuendelea kutekeleza sera ya fedha.

**d) Akiba ya Fedha za Kigeni**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Juni, 2023 akiba ya fedha za kigeni ilifikia **dola ya Marekani milioni 5,282.6** ikilinganishwa na **dola ya Marekani milioni 5,110.3** mwezi Juni 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 3.37**. Kiasi hicho kingeweza kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban **miezi 4.8**. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la akiba kukidhi **miezi 4.0** na zaidi ya lengo la **miezi 4.5** kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na akiba inayozidi malengo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuchochea uzalishaji wa bidhaa za ndani ili kupunguza uagizwaji wa bidhaa kutoka nje na kulinda akiba yake ya fedha za kigeni na kujikinga na mvurugiko wa mnyororo wa ugavi kwa zile bidhaa tunazotegemea kuagiza kutoka nje ya nchi. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupitia Benki Kuu kununua dhahabu na kuihifadhi kama sehemu ya akiba ya fedha za kigeni.

**e) Deni la Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Juni 2023, deni la Serikali lilikuwa **shilingi trilioni 80.33** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 71.56** katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la **shilingi trilioni 8.77** au **asilimia 12.43.** Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa **shilingi trilioni 51.4** na deni la ndani lilikuwa **shilingi trilioni 28.93**. Ongezeko la deni limetokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023 mapato ya ndani yaliyokusanywa ukitoa mapato ya Halmashauri ni **shilingi trilioni 25.3.** Kamati ilibaini kati ya fedha hizo, **shilingi**

**trilioni 10.09** zilitumika kulipa deni sawa na **asilimia 39.95.** Hivyo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Serikali kupima uhimilivu wa deni kwa kutumia kiashiria cha makusanyo ya mapato ya ndani kwa ulipaji wa deni kwa kuwa Serikali hutumia takribani **asilimia 40** ya mapato ya ndani kulipa deni; na

ii. Serikali kulipa riba kwa wakati hususan kwa mikopo ya kibiashara ili kuepukana na athari zinazoweza kujitokeza kama kuongezeka kwa riba inayotokana na adhabu ya ucheleweshaji na nchi kuwa na taswira mbaya kwenye soko la fedha la kimataifa hali inayoweza kupelekea kutopata mikopo kwa urahisi.

### 2.1.2. Mwenendo wa Mapato na Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia **shilingi trilioni 41.48**. Hadi kufikia Juni, 2023 Serikali ilikusanya **shilingi trilioni 38.98** kutoka vyanzo vya ndani na nje, sawa na **asilimia 94.0** ya lengo la mwaka. Kati ya fedha zilizokusanywa, **shilingi trilioni 26.88** zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi trilioni 13.97** zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo zilizotolewa, **shilingi trilioni 12.26** ni fedha za ndani na **shilingi trilioni 1.71** ni fedha za nje. Tofauti ya mapato na ridhaa ya matumizi iliyotolewa ya **shilingi trilioni 1.878** iligharamiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu (*overdraft*).

**Jedwali Na. 1. Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 na Mwaka 2022/23 (Shilingi Bilioni)**

| | 2021/22 | | | 2022/23 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Bajeti** | **Halisi** | **%** | **Bajeti** | **Halisi** | **%** |
| **Mapato ya Ndani** | **25,691.70** | **24,395.60** | **95** | **28,017.87** | **26,277.89** | **93.80** |
| Mapato ya kodi | 20,283.40 | 20,029.30 | 99 | 22,011.63 | 21,395.30 | 97.20 |
| Mapato yasiyo ya kodi(TRA) | 1,494.70 | 902.00 | 60 | 1,648.44 | 1,214.90 | 73.70 |

| | 2021/22 | | | 2022/23 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Bajeti** | **Halisi** | **%** | **Bajeti** | **Halisi** | **%** |
| Mapato yasiyo ya kodi | 3,049.80 | 2,574.80 | 84 | 3,352.82 | 2,646.69 | 78.90 |
| Mapato ya Halmashauri | 863.90 | 889.50 | 103 | 1,012.29 | 1,021.04 | 100.90 |
| **Misaada** | **1,138.10** | **708.50** | **62** | **1,101.49** | **596.38** | **54.10** |
| Misaada ya Kibajeti | | 103.20 | 0 | | | |
| Misaada ya Kimaendeleo | 915.50 | 519.30 | 57 | | | |
| Mifuko ya Kisekta | 222.60 | 86.00 | 39 | | | |
| **Mikopo Nafuu** | **3,128.50** | **4,116.80** | **132** | **3,547.07** | **2,966.48** | **83.60** |
| Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 1,310.70 | 1,291.70 | 99 | | | |
| Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo | 1,770.00 | 2,818.30 | 159 | | | |
| Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta | 47.80 | 6.80 | 14 | | | |
| **Mikopo ya Kibiashara Kutoka Nje** | **3,045.10** | **1,809.50** | **59** | **3,034.00** | **3,011.73** | **99.30** |
| **Mikopo ya Kibiashara Kutoka Ndani** | **4,989.10** | **5,894.40** | 118 | **5,780.15** | **6,124.51** | **106.00** |
| Mikopo ya Kugharamia Miradi | 1,838.80 | 2,850.00 | 155 | 2,480.15 | 2,610.60 | 105.30 |
| Mikopo ya Kulipa Mtaji Deni la Ndani | 3,150.30 | 3,044.40 | 97 | 3,300.00 | 3,513.91 | 106.50 |
| **JUMLA YA MAPATO** | **37,992.50** | **36,924.80** | **97** | **41,480.58** | **38,976.99** | **94.00** |
| **Matumizi ya Kawaida** | **22,732.80** | **22,561.00** | **99** | **26,474.58** | **26,882.59** | **101.50** |
| Mishahara | 8,136.50 | 8,087.40 | 99 | 9,830.75 | 9,046.21 | 92.00 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali (Deni) | 8,756.80 | 8,756.80 | 100 | 11,308.36 | 11,951.43 | 105.70 |
| Matumizi Mengineyo & CFS | 5,839.50 | 5,717.30 | 98 | 5,335.46 | 5,884.96 | 110.30 |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **15,259.70** | **14,654.30** | **96** | **15,006.00** | **13,970.71** | **93.10** |
| Miradi ya Fedha za Ndani | 11,591.10 | 11,554.60 | 100 | 2,306.92 | 12,259.08 | 99.60 |
| Miradi ya Fedha za Nje | 3,668.60 | 3,099.70 | 84 | 2,699.08 | 1,711.62 | 63.40 |
| **JUMLA YA MATUMIZI** | **37,992.50** | **37,215.80** | **98** | **41,480.58** | **40,853.30** | **98.50** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwani katika kipindi cha uongozi wake kumekuwa na ongezeko la

fedha kutoka kwa Wafadhili na ukusanyaji wa mapato ya ndani. Hata hivyo, ili kuongeza ufanisi zaidi katika utekelezaji wa bajeti Kamati inashauri yafuatayo:-

i. Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) iendelee kuimarisha mifumo yake na kuhakikisha kuwa inasomana ili kuwezesha mapato mengi kukusanywa kwa ufanisi na kupunguza mianya ya upotevu pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa Umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari;

ii. Kwa upande wa Mapato yasiyo ya kodi kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Kamati inaishauri Serikali kuweka mifumo mizuri na rafiki ya ulipaji wa ada na tozo mbalimbali, kufanya mapitio ya sheria zinazosimamia ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi ili kuhakikisha zina akisi hali ya sasa pamoja na kupitia upya viwango vya ada na tozo vinavyolalamikiwa na wananchi na hivyo kusababisha kukwepa kulipa kodi na tozo;

iii. Kwa kuwa gharama za mashine za EFD ni kati ya **shilingi 500,000 hadi milioni 10** kutegemeana na aina ya biashara, gharama hizi zinaweza kuwa juu kwa baadhi ya wafanyabiashara wadogo. Hivyo, Serikali itathmini uwezekano wa kununua na kugawa bure mashine za EFD kwa wafanyabiashara wasiotunza mahesabu. Hatua hii itaisaidia Serikali kukusanya taarifa muhimu za mauzo na kodi stahiki; na

iv. Serikali ifanye marekebisho ya Sheria zenye ombwe ambazo zinasababisha kuwepo na muamko mdogo wa matumizi ya vifaa vya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato kwa Wizara, Idara, Wakala, Taasisi na Mamlaka za Serikali.

### 2.1.3. Masuala yaliyobainika kwenye Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/23

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/23, Kamati ilibaini mapungufu yafuatayo: -

#### 2.1.3.1. Maombi ya Fedha nje ya Fungu

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23, Kamati imebaini uwepo wa changamoto ya maombi ya fedha nje ya bajeti na kuathiri Bajeti ya Serikali. Aidha, Kamati imebaini maombi haya yanatokana na mapungufu katika upangaji wa bajeti kwa kutozingatia vipaumbele, na hivyo matumizi ya msingi kutokupangwa katika bajeti ili yaombewe bajeti ya ziada. Serikali ihakikishe uhamisho wa fedha uwe katika maeneo ya dharura tu na sio maeneo yaliyopaswa kutengewa bajeti.

#### 2.1.3.2. Miradi ya Maendeleo kutokamilika kwa Wakati

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kuna hati za madai za wakandarasi, watoa huduma na wazabuni hazijalipwa hivyo kusababisha baadhi ya miradi ama kutokamilika kwa wakati au kusimamisha utekelezaji. Changamoto hii imekuwa na athari zifuatazo: -

i. Gharama za Miradi kuongezeka tofauti na fedha zilizotengwa kwenye makisio ya Bajeti;

ii. Maombi ya fedha nje ya Bajeti na hivyo kuathiri shughuli nyingine zilizopangwa katika mwaka husika;

iii. Bakaa ya madai ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma wa miaka ya nyuma kutolipwa katika mwaka husika wa fedha na hivyo kuathiri ulipaji wa hati za madai kwa miaka unayofuata; na

iv. Muda mrefu wa Uhakiki wa madeni ya watumishi, wazabuni, wakandarasi na watoa huduma na hivyo

kusababisha madeni ya mwaka mmoja wa fedha kulipwa mwaka unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha hati za madai za wakandarasi, watoa huduma na wazabuni zinahakikiwa na kulipwa kwa wakati.

### 2.1.3.3. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23 Serikali ilipanga kutumia **shilingi trilioni 15** kwa ajili matumizi ya maendeleo. Hadi Juni 2023, fedha zilizotumika ni **shilingi trilioni 13.97 sawa na asilimia 93.7 ya lengo.** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa kati ya fedha hizo zilizotumika katika matumizi ya maendeleo, **shilingi trilioni 12.26** ni fedha za ndani sawa na **asilimia 87.76** na **shilingi trilioni 1.71** ni fedha za nje sawa na **asilimia 12.24**. Kamati inampongeza **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa utolewaji huu wa fedha za maendeleo. Hatua hii inadhihirisha utayari wake katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati kuhusu matumizi ya maendeleo umebaini kwamba kuna baadhi ya mafungu yamepokea fedha zaidi ya **asilimia 100** na kuna mafungu yamepokea fedha chini ya **asilimia 50**. Mafungu yaliyopokea zaidi ya **asilimia 100** ni fungu **05** (Tume ya Taifa ya Umwagiliaji)**, 06** (Mkaguzi Mkuu wa Ndani)**, 57** (Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa)**,36** (Katavi)**, 71** (Pwani) na **99** (Wizara ya Mifugo na Uvuvi) na mafungu yaliyopokea chini ya **asilimia 50 Fungu 45** (Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi)**, 33** (Sekretarieti ya Maadili). Hivyo, ni dhahiri kwamba kuna baadhi ya miradi na shughuli hazikutekelezwa kutokana na uhamisho huu wa fedha wa zaidi ya **asilimia 100**.

Hivyo, kuna haja ya Serikali kujielekeza zaidi katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vyanzo vyetu vya ndani ili kuhakikisha miradi iliyokusudiwa inakamilika kwa wakati na kuepuka kusababisha ongezeko la gharama. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia uwiano sahihi kwenye kupeleka fedha za matumizi kulingana na bajeti.

#### 2.1.4. Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ulitengewa jumla ya **shilingi trilioni 15.01** sawa na **asilimia 36.18** ya Bajeti ya Serikali. Hadi mwezi Juni 2023 jumla ya **shilingi trilioni 13.97** zilikuwa zimetolewa sawa na **asilimia 93.1**. Kamati ilichambua na kujadili utekelezaji wa Mpango huo, ukiwa ni Mpango wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa 2021/22 – 2025/26 uliobeba Dhima ya ***"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitoa ushauri ufuatao kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo: -

a) Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi za Umma kushirikiana wakati wa kupanga na kutekeleza miradi ili kupunguza gharama na kupunguza miradi inayofanana kutekelezwa na Taasisi zaidi ya moja;
b) Serikali kujielekeza zaidi kwenye mikopo ya masharti nafuu na ya kati katika utekelezaji wa miradi ili kuepuka matumizi ya mikopo ya kibiashara ambayo ina riba za juu na inaiva katika kipindi cha muda mfupi;
c) Upembuzi yakinifu wa miradi ufanyike pindi Serikali ikiwa na nia ya kuanza kutekeleza miradi hiyo;
d) Kipaumbele kitolewe kwa miradi yenye manufaa ya kiuchumi na kijamii;
e) Kupima uwezo wa wakandarasi kabla ya kuwapa zabuni za ujenzi au utekelezaji wa miradi;

f) Ulipaji wa madeni ya wazabuni ufanyike kwa wakati ili kuepuka gharama za riba zinazotokana na ucheleweshaji wa malipo;
g) Serikali kulipa fidia kwa wakati kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi;
h) Serikali ikamilishe miradi ya kielelezo ya muda mrefu ambayo haijakamilika;
i) Miradi yenye sura ya kibiashara itekelezwe kwa Mfumo wa Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP);
j) Kuhakikisha kwamba miradi ya madini adimu inatekelezwa kwa wakati ili matumizi yake yasipitwe na wakati na hivyo kushindwa kuliletea Taifa manufaa;
k) Kuanzisha utaratibu maalumu wa kusamehe ada za leseni kwa miradi ambayo inatekelezwa na Taasisi moja ya Serikali na inatakiwa kulipwa kwa Taasisi nyingine ya Serikali;
l) Kuandaa miundombinu ya msingi kabla ya kuanza kutekeleza mradi; na
m) Serikali kupitia Tume ya Mipango kuanzisha kitengo mahsusi cha kusanifu na kuhakiki ubora wa miradi iliyosanifiwa ili kukabiliana na changamoto ya usanifu duni;

## 2.2. Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023 (The Finance Bill, 2023)

**Mheshimiwa Spika,** Muswada uliowasilishwa na Serikali ulikuwa na jumla ya Sheria kumi na nane (18), Kamati ilichambua na kujadili Ibara zote za Muswada pamoja na kupokea maoni kutoka kwa wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Baada ya kukamilisha uchambuzi na kupokea maoni ya wadau, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali na kuwasilisha Bungeni Taarifa ya maoni na ushauri kuhusu Muswada huo kwa mujibu wa Kanuni ya 127 (1). Sheria zilizofanyiwa mabadiliko ni: -

i. Sheria ya Hakimiliki na Hakishirikishi, Sura ya 218;
ii. Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306
iii. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
iv. Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196;

v. Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249
vi. Sheria ya Ushuru wa Magari, Sura ya 84;
vii. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
viii. Sheria ya kodi ya Mapato, Sura ya 332;
ix. Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;
x. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
xi. Sheria ya Kodi ya Majengo ya Serikali za Mitaa, Sura ya 289;
xii. Sheria ya Madini, Sura ya 123;
xiii. Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Sura ya 437;
xiv. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220;
xv. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;
xvi. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148;
xvii. Sheria ya Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82; na
xviii. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Sheria hizi umefafanuliwa kwa kina katika Sehemu ya Nne ya Taarifa hii.

### 2.3. Tathmini ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/25 pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mpango wa Mendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/25 pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/25 mwezi Novemba, 2023 kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura 439. Kamati ya Bajeti ilichambua, ikajadili na ikatoa mapendekezo kwa Serikali kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 47.42**. kati ya fedha hizo, **shilingi trilioni 34.44** ni mapato ya ndani, **shilingi bilioni 690.9** ni misaada kutoka katika vyanzo mbalimbali, **shilingi trilioni 6.16** ni mikopo kutoka nje na **shilingi trilioni 6.14** ni mikopo ya ndani kwa

ajili ya kudumisha deni na mikopo ya ndani ya kibiashara. Kati ya fedha hizo Serikali imepanga kutumia **shilingi trilioni 32.1** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi trilioni 15.32** kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Maendeleo imeongezeka kutoka **shilingi trilioni 14.08** mwaka 2023/24 hadi **shilingi trilioni 15.33** mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la **asilimia 8.8 (shilingi trilioni 1.25)**. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuhakikisha kwamba inatenga kati ya **asilimia 30** hadi **40** ya Bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati iliishauri Serikali kuhusu masuala yafuatayo: -

### 2.3.1. Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Utekelezaji wa Mpango

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Tatu wa Miaka Mitano umebainisha kwamba sekta binafsi katika mwaka wa fedha 2024/25 inatarajiwa kuchangia kiasi cha **shilingi trilioni 12.30.** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba hakuna mfumo wa kutunza Taarifa za uwekezaji wa rasilimali fedha zilizowekezwa na sekta binafsi. Mfano, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, hakuna Taarifa yoyote inayoonyesha kiasi cha fedha kilichowekezwa na sekta binafsi katika utekelezaji. Aidha, hakuna mchanganuo wa mgawanyo wa uwekezaji huu kwa sekta mbalimbali,

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za umma na Binafsi kuweka mfumo utakaosaidia kupata takwimu hizo muhimu ili zitumike katika ufanyaji wa tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano.

### 2.3.2. Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi za Umma Kutoshirikiana wakati wa Kupanga na Kutekeleza Miradi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba Wizara, Idara na Taasisi za Umma hazina ushirikiano katika utekelezaji wa miradi. Hali hii imesababisha baadhi ya Taasisi kutekeleza miradi katika ngazi ya Serikali za Mitaa lakini uratibu na

usimamizi hufanywa Serikali Kuu na hivyo miradi kukosa uangalizi na kutekelezwa chini ya kiwango.

**Mheshimiwa Spika,** mfano Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira. Wizara zote hizi zinachimba mabwawa na visima kwa matumizi tofauti, mfano mabwawa ya kilimo, uvuvi na umwagiliaji. Miradi hii inaweza kutekelezwa na Wizara moja ya maji na bwawa hilo likatumika kwa shughuli za kilimo, uvuvi na umwagiliaji. Kamati iliishauri Serikali kwamba Wizara zinapotekeleza miradi ambayo inashabihiana, wahusika wote washirikishwe na Fedha zitengwe kupitia Fungu moja kuliko kutawanya fedha kidogo kidogo katika mafungu mengi na kuwa na miradi ambayo haina tija.

### 2.3.3. Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba mwongozo wa uandaaji wa Bajeti unaotolewa na Serikali kila mwaka huwa hauambatani na Ukomo wa Bajeti kwa kila Fungu. Hali hii husababisha ukomo wa bajeti kwa mafungu mbalimbali kutolewa mwezi Machi, kila mwaka mara baada ya Mpango na Mwongozo kuwasilishwa Bungeni. Hatua hii hulazimu baadhi ya Maafisa Masuuli kubadili bajeti zao na kuandaa vitabu kwa ajili ya Kamati za Bunge, vinavyoendana na ukomo uliotolewa na ratiba hiyo. Utaratibu huu umekuwa na madhara kwa Serikali za Mitaa hasa pale ambapo bajeti zake zinakuwa zimekwisha pitishwa na vikao vyote vya Halmashauri na kikao cha Ushauri wa Mkoa (RCC).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kutoa ukomo wa Bajeti sambamba na mapendekezo ya mpango ili bajeti zitakazoidhinishwa katika Serikali za Mitaa zisifanyiwe mabadiliko isipokuwa kama kuna ongezeko.

### 2.4. Hoja Mahsusi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishughulikia hoja mahsusi 27 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 na 124 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

#### 2.4.1. Hoja zilizotokana na Kamati za Bunge za Kisekta (Kanuni ya 117)

**Mheshimiwa Spika,** Hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2022/23 na makadirio ya matumizi kwa mwaka 2023/24 katika ngazi ya Kamati za Kisekta kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (3) ni kama zifuatazo:-

a) Utolewaji wa Barua ya Muamana (*Letter of Credit*) kwa Kampuni ya Taifa ya Mbolea (TFC) ili iweze kuagiza mbolea kwa wakati kuendana na msimu wa kilimo;
b) Kupitia upya muundo wa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU) pamoja na kufanya mabadiliko ya Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu ili kuendana na miundo ya Kimataifa;
c) Kuongeza fedha kwa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kwa ajili ya ukarabati wa barabara zilizoharibika kutokana na mvua; na
d) Mahitaji ya fedha za mishahara kwa watumishi wa Hospitali ya CCBRT.

#### 2.4.2. Hoja zilizotokana na Mjadala Bungeni wakati wa Kujadili Bajeti za Wizara (Kanuni ya 124)

**Mheshimiwa Spika,** Hoja zilizotokana na mjadala wa utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka 2022/23 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2023/24 kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1) ni kama ifuatavyo: -

a) **Uagizaji wa Mafuta ghafi ya Mchikichi (*Crude Palm Oil*) kutoka nje pamoja na Uzalishaji wa Mafuta ya kula Nchini kutokana na mbegu za Pamba, Michikichi na Alizeti**

**Mheshimiwa Spika**, mwaka 2022 Serikali kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ili kupunguza ushuru wa Forodha wa uagizaji wa

mafuta ghafi ya Mchikichi (Crude Palm Oil) kutoka **asilimia 25** hadi **asilimia 0**, kwa lengo kusaidia viwanda vya ndani vinavyo chakata mafuta ya Mchikichi (Crude Palm Oil) vipate malighafi na kusaidia upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa bei nafuu. Kwa upande mmoja hatua hizi zilileta manufaa kwa upatikanaji wa mafuta ya kula nchini na kwa upande mwingine zilisababisha wakulima wa zao la alizeti kukosa soko la zao hilo.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia changamoto hiyo Kamati ilitoa mapendekezo yafuatayo: -

i. Kuanzisha utaratibu wa kutoa vibali vya uagizaji wa mafuta ya kula kwa kulinganisha na mahitaji *(Import quota permit);*
ii. Kuendelea na utaratibu wa kutoza kwa kiwango cha **asilimia 0** cha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa mafuta yanayotokana na mbegu za ndani yaliyochujwa mara mbili (*Double Refined*) kwa sababu hatua hii itachochea uzalishaji wa mafuta ndani ya nchi; na
iii. Viwanda vya ndani ambavyo vinachakata mafuta ghafi ya Mchikichi (*Crude Palm Oil*) na kuyauza nje ya nchi viwekewe utaratibu maalum wa kuviwezesha kuingiza mafuta hayo, kuyachakata na baada ya kuyauza vithibitshe mauzo ya mafuta hayo nje ya nchi. Hatua hii itazuia mafuta yanayozalishwa nchini kwa lengo la kuuzwa nje ya nchi kuuzwa ndani ya nchi;

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilipokea mapendekezo hayo na kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wizara ya Mipango na Uwekezaji na Wizara ya Viwanda na Biashara inafanyia kazi utaratibu utakaoongeza udhibiti zaidi kwa viwanda vinavyochakata mafuta ghafi ya chikichi yaliyoagizwa kutoka nje ya nchi kwa lengo la kuchakata na kuuza nje (re export) ili kuhakikisha mafuta hayo hayauzwi hapa nchini. Aidha, mbinu za kiforodha zitatumika ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuwa na utaratibu wa kuzalisha chini ya ghala la kiforodha (bonded warehouse). Vilevile, Serikali ilikubali kuendelea kutoza kiwango cha

**asilimia 0** cha Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mafuta yanayotokana na mbegu za ndani yaliyochujwa mara mbili.

b) **Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA)**
**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na changamoto ya wanyamapori kuvamia na kudhuru binadamu pamoja na kufanya uharibifu katika makazi na mashamba ya wananchi. Kutokana na changamoto ya uwezo mdogo wa kifedha, rasilimali watu pamoja na vifaa, TAWA inashindwa kuzuia na kudhibiti wanyamapori waharibifu ipasavyo. Vilevile, Kamati ilibaini kwamba mahitaji halisi ya bajeti ya TAWA kwa mwaka 2023/24 ni **shilingi bilioni 178.18** na ukomo wa bajeti ulikuwa ni **Shilingi bilioni 128.69,** hivyo kuna nakisi ya s**hilingi bilioni 49.49** ukilinganisha na mahitaji.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto hizo, Kamati iliishauri Serikali yafuatayo;

i. Kutenga **shilingi bilioni *9.93*** kwa ajili ya ununuzi wa helikopta ndogo aina ya *H.125 Airbus* yenye uwezo wa kupaa katika anga la chini (low altitude) kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori waharibifu; na

ii. Kuongeza Bajeti ya matumizi mengineyo ya TAWA kwa **shilingi bilioni 5** ili kuongeza uwezo wa Mamlaka kudhibiti maeneo yenye changamoto kubwa ya Wanyamapori waharibifu.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubali ushauri wa Kamati na katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) imepanga kununua helikopta moja aina ya Robinson R 44 Raven II yenye uwezo wa kupaa katika anga la chini (low altitude) ambayo itatumiwa kwenye hifadhi ya Taifa ya Serengeti na maeneo yanayosimamiwa na TAWA.

c) **Utozaji wa Ushuru wa Forodha kwa Bidhaa ya Kitenge**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kwamba bidhaa ya kitenge kwa mujibu wa Protokali ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, imewekwa kwenye kundi la bidhaa nyeti (*Sensitive Item*). Aidha, Kamati ilibaini kwamba changamoto kubwa zinazoikabili bidhaa ya kitenge nchini ni viwanda vya ndani kutokuwa na uwezo wa kuzalisha vitenge vya kutosha na vyenye ubora pamoja na gharama za kuingiza vitenge Tanzania kuwa kubwa. Bidhaa hii inatozwa ushuru wa forodha wa **dola ya Marekani 0.5** kwa mita, tozo ya **dola ya Marekani 0.8** kwa mita kwa kitenge cha pamba na tozo ya **dola ya Marekani 0.7** kwa mita kwa kitenge cha *polyester* kinapofika nchini. Gharama hizi ni kubwa ukilinganisha na nchi zinazotuzunguka za Kenya, Malawi, Zambia, Uganda na Tanzania Zanzibar. Hali hii huchochea biashara ya magendo mipakani na kuikosesha Serikali Mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali, na Serikali ilikubali kushusha viwango vinavyotozwa katika thamani ya vitenge vinapofika nchini (*Cost Insurance and Freight-CIF*) kwa vitenge vya pamba kutoka **dola ya Marekani 0.8** kwa mita hadi **dola ya Marekani 0.4** kwa mita na Vitenge vya *polyester* kutoka **dola ya Marekani 0.7** kwa mita hadi **dola ya Marekani 0.36** kwa mita. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kuweka utaratibu maalum utakaosaidia viwanda vya ndani vipate pamba kwa mwaka mzima ili visiagize nyuzi za pamba (*yarn)* kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipokea ushauri wa Kamati, ambapo kupitia hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2023/24, Serikali ilipunguza ushuru wa forodha kutoka kiwango cha **asilimia 50** hadi **asilimia 35** kwenye vitenge vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi ikiwa ni hatua muhimu katika kutoa unafuu. Aidha, kuhusu utaratibu maalum wa ununuzi na upatikanaji wa pamba kwa mwaka mzima katika viwanda vya ndani, Serikali inaendelea kulifanyia kazi

pendekezo hili ili kuja na hatua nzuri za kukabiliana na changamoto iliyopo hivi sasa.

**d) Changamoto ya upatikanaji wa Fedha za Kigeni nchini**

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto ya uhaba wa fedha za kigeni uliochangiwa na sababu mbalimbali, Kamati iliishauri Serikali masuala yafuatayo;

i. Malipo yote yanayofanyika ndani ya nchi yafanyike kwa shilingi za Kitanzania mfano ada za shule za Kimataifa, kodi za nyumba, malipo ya wafanyakazi wa sekta binafsi hoteli na malipo ya huduma zinazotolewa na makampuni ya ndani;
ii. Kufanya uchambuzi na kubaini bidhaa ambazo si za msingi na zinaagizwa kwa wingi kutoka nje kuziongezea kodi ili kupunguza uagizwaji wake;
iii. Kuangalia upya utozaji wa kodi kwa sekta ya utalii ili kuvutia watalii wengi zaidi;
iv. Kuharakisha mchakato wa Benki Kuu kununua na kutunza dhahabu kama akiba fedha (Gold reserve);
v. Kuongeza thamani na mauzo nje kwa bidhaa za asili; na
vi. Malighafi za miradi inayotekelezwa na Serikali zinunuliwe kutoka ndani na endapo hazipatikani ndipo ziagizwe kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipokea ushauri wa Kamati, na kwa sasa Serikali imeanzisha zoezi la kununua dhahabu kama akiba ya fedha za kigeni. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuongeza thamani ya bidhaa na mazao ya asili.

**e) Mfumo wa Stempu za Kodi za kielektroniki *(Electronic Tax Stemp-ETS)***

**Mheshimiwa Spika,** mfumo wa Stempu za Kodi za Kielektroniki (ETS) umekuwa unalalamikiwa na wafanyabiashara wa ndani hususan wazalishaji wa vinywaji na sigara kutokana na gharama kubwa. Gharama hizo

zimesababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kwa wafanyabiashara. Aidha, ilibainika kuwa gharama ya stempu moja ni kubwa kuliko ushuru wa bidhaa *(Excise duty)* inayotozwa katika baadhi ya bidhaa na Serikali. Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kupunguza viwango vya ushuru wa stempu kwa kushauriana na muwekezaji anayemiliki na kuendesha mfumo uliopo. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ushuru wa stempu umepungua kati ya **asilimia 14** hadi **asilimia 34** chini ya punguzo la **asilimia 75** lililopendekezwa na Shirikisho la Wamiliki wa Viwanda (Confideration of Tanzania Industries - CTI).

**Jedwali Na. 2 Ulinganisho wa Bei za Stempu za Kieletroniki *(Electroniki Tax Stamp)***

| Na. | Aina ya Bidhaa | Chanzo | Bei ya zamani kwa stempu'1000' | Bei mpya kwa stempu '1000' | Punguzo Kwa asilimia(%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Pombe kali, na pombe kali za mvuke | Zote | 42,214.37 | 33,392.00 | -20.90 |
| 2 | Mvinyo wa zabibu n.k | Zote | 42,214.37 | 33,392.00 | -20.90 |
| | Mvinyo wa matunda kama vile ndizi na nyanya n.k | Wenye matunda ya ndani kwa asilimia 75% au zaidi | 17,435.37 | 11,482.00 | -34.15 |
| 3 | Sigara au bidhaa mbadala wa tumbaku | Zote | 42,214.37 | 29,854.00 | -29.28 |
| | Bidhaa nyingine za tumbaku n.k | Zote | 42,214.37 | 29,854.00 | -29.28 |
| 4 | Bia n.k | Zinazozalishwa nchini | 18,312.91 | 14,857.00 | -18.87 |
| | Bia iliyotengenezwa kwa kimea n.k | Zinazoingizwa kutoka nje | 23,093.20 | 17,795.00 | -22.94 |
| 5 | Juisi za matunda na mbogamboga | Zinazozalishwa nchini (kwa matunda ya ndani) | 8,082.62 | 6,889.00 | -14.77 |
| | Juisi ya matunda ikiwemo ya zabibu, juisi ya | Zinazoagizwa kutoka nje | 15,264.51 | 10,068.00 | -34.04 |

| Na. | Aina ya Bidhaa | Chanzo | Bei ya zamani kwa stempu'1000' | Bei mpya kwa stempu '1000' | Punguzo Kwa asilimia(%) |
|---|---|---|---|---|---|
| | mbogamboga zisizowekwa chachu | | | | |
| 6 | Maji ya chupa | Zote | 8,082.62 | 6,889.00 | -14.77 |
| 7 | Vinywaji vilaini au maji yaliyoongezewa ladha na vinywaji vingine visivyo na kilevi bila kujuisha juisi za matunda | Zilizo chini ya Tarrif namba 2202.10.00 | 8,082.62 | 6,889.00 | -14.77 |
| | Vinywaji vilaini au maji yaliyoongezewa ladha na vinywaji vingine visivyo na kilevi bila kujuisha juisi za matunda | Vinywaji vingine chini ya tarrif namba 2202.91.00 na 2202.99.00 | 15,264.81 | 10,068.00 | -34.04 |
| 8 | Bidhaa za filamu na muziki (Yaan CDLVCDsldvdlkanda zilizorekodiwa | Zote | 16,165.24 | 16,165.24 | 0.00 |

***Chanzo:*** *Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)*

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto hiyo Kamati ilipendekeza masuala yafuatayo kwa Serikali;

i. Mamlaka ya Mapato ibainishe mkakati wake wa muda mfupi na mrefu wa namna ya kuendesha na kumiliki mfumo huo; na
ii. Kuanzisha upya mchakato wa kumpata mzabuni wa kutoa huduma ya Stempu za Kielektroniki;

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na kuunda timu shirikishi kwa lengo la kutembelea Makampuni mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kutafuta na kupata mfumo bora na wa gharama nafuu.

**f) Mradi wa Uboreshaji wa Milki ya Ardhi (LTP)**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Tanzania ilipata Mkopo wa miaka 4 wa **Dola ya Marekani milioni 150** sawa na wastani wa **shilingi bilioni 351.77** kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya

matumizi bora ya ardhi ikiwemo upimaji, urasimishaji wa ardhi na ugawaji wa hati, mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2022/23. Kamati ilipitia mgawanyo wa fedha hizo na kubaini kwamba baadhi ya matumizi yake hayatakuwa na manufaa ya muda mrefu kwenye sekta ya ardhi. Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kwa kuwa majukumu mengine ya mkopo huo ni ya kawaida katika utekelezaji wa shughuli za Serikali, ni vyema Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi itengewe jumla ya shilingi **bilioni 30** kwa muda wote wa mradi ili iweze kupima vijiji 1200 kwa gharama ya **shilingi milioni 25** kwa kila kijiji.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipokea mapendekezo ya Kamati na kufanya mapitio kwa baadhi ya vipengele vya mradi na kuongeza idadi ya vijiji vitakavyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi ili kupunguza migogoro ya ardhi nchini.

**g) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2023/24 Fungu **91**, lilihitaji nyongeza za fedha ya **shilingi bilioni 12.46** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya msingi ya operesheni mbalimbali za udhibiti na ukamataji wa dawa za kulevya baharini, katika viwanja vya ndege na nchi kavu. Baada ya Kamati kufanya uchambuzi, ilipendekeza Fungu hili liongezewe **shilingi bilioni 10.46.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kuahidi kuangalia uwezekano wa kugharamia upungufu wa kibajeti utakaojitokeza katika kipindi cha nusu mwaka cha mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali mwezi Desemba, 2023. Hata hivyo, Kamati ilibaini mpaka hadi kufikia mwezi Januari, 2024 hakuna fedha zilizotolewa kwa mamlaka hiyo.

### 2.5. Ziara za Kamati za Kukagua Miradi ya Maendeleo pamoja na mafunzo

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati ilifanya ziara katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam,

Arusha, Manyara, Singida, Tabora, Iringa, Dodoma na Kilimanjaro. Ziara hizo zilikuwa na malengo yafuatayo: -

i. Kukagua miradi ya maendeleo na kupokea Taarifa za Utendaji kazi wa Taasisi zinazosimamiwa na Kamati;
ii. Kukagua miradi ya maendeleo ya kimkakati (Strategic/Flagship Projects);
iii. Kukagua endapo miradi iliyotekelezwa inaendana na thamani halisi ya fedha;
iv. Kubaini endapo kuna changamoto zozote za kifedha, kiutendaji, kiuendeshaji pamoja na ufanisi katika utekelezaji; na
v. Endapo matakwa ya Sheria ya Bajeti Sura 439 yamefuatwa kikamilifu katika utekelezaji wa miradi pamoja na usimamizi wa fedha za umma

### 2.5.1. Masuala muhimu yaliyojitokeza

#### 2.5.1.1. Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP)

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere ukikamilika unatarajiwa kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa **Megawati 2,115**. Kiwango hiki cha uzalishaji kitakuwa ni kikubwa kuliko vyanzo vyote vya umeme vilivyopo nchini hivi sasa. Gharama ya mradi ni **shilingi trilioni 6.56.** Hadi kufikia mwezi Julai, 2023 jumla ya **shilingi trilioni 5.53** zilikuwa zimetumika sawa na **asilimia 84.35** ya fedha zote za mradi**.** Aidha, malipo yaliyofanyika ni sawa na **asilimia 100** ya malipo yaliyoidhinishwa kulingana na utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kupokea Taarifa ya Mradi pamoja na kukagua utekelezaji wake Kamati ilishauri masuala yafuatayo: -

i. Kabla ya mkandarasi kukamilisha na kukabidhi mradi kuhakikisha anahamisha ujuzi na utaalamu kwa watanzania walioko eneo la mradi (*technology transfer)* ili waweze kuendesha mitambo na mfumo

wote wa uzalishaji wa umeme pindi mkandarasi atakapomaliza kazi yake;

ii. Kuangalia uwezekano wa kuajiri baadhi ya vijana walioshiriki katika ujenzi wa mradi kwa maeneo ambayo wamepata ujuzi wa kutosha;

iii. Serikali kuhakikisha inadhibiti upotevu wa umeme kutoka **asilimia 15** ya sasa hadi viwango vya upotevu vinavyokubalika kimataifa ambavyo ni **asilimia 8 - 9**;

iv. Serikali ihakikishe kwamba jamii inayozunguka maeneo ya mradi inanufaika na mchango wa hisani kwa jamii (Corporate Social Responsibility CSR);

v. Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati kushirikiana katika kutunza mazingira ya vyanzo vya maji vya mto Rufiji ili kuhakikisha bwawa linapata maji ya kutosha muda wote na kuendelea kuhifadhi viumbe maji vilivyopo; na

vi. Kuimarisha usalama wa eneo la mradi ili kuwalinda wafanyakazi na familia zao dhidi ya wanyama wakali kwa kujenga uzio katika makazi ya wafanyakazi.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilikubali kuyafanyia kazi mapendekezo hayo ya kamati na mengine tayari yalikuwa yamezingatiwa wakati mradi unabuniwa.

**2.5.1.2. Miradi ya Ujenzi wa Mabwawa ya Umwagiliaji pamoja na Mashamba ya Mbegu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea miradi ya mabwawa ya umwagiliaji katika Mikoa ya Dodoma, Manyara, Arusha, Singida, Tabora na Iringa yenye thamani ya zaidi ya **shilingi bilioni 100.** Lengo la ziara hiyo ilikuwa ni kukagua utekelezaji wa miradi hiyo inayotekelezwa chini ya mkopo wa ECF (Extended Credit Facility). Miradi hii ikikamilika itasaidia kuongeza ukubwa wa eneo la umwagiliaji na kupunguza kilimo cha kutegemea mvua. Baada ya Ziara Kamati iliishauri Serikali masuala yafuatayo: -

i. Kukamilisha miradi kwa wakati ili kupunguza gharama za ujenzi ambazo zinaweza kuongezeka kutokana na kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo;
ii. Kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi wote wanaostahili kulipwa fidia;
iii. Kuhakikisha inawasimamia wakulima watakao gawiwa maeneo ili wafanye kilimo chenye tija; na
iv. Juhudi hizi za ujenzi wa mabwawa ziende sambamba na utafutaji wa masoko ya mazao ndani na nje ya nchi ili pindi uzalishaji utakapoanza kusiwe na changamoto ya masoko.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile, Kamati iliishauri Serikali kutenga Bajeti ya kutosha kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania *(Tanzania Agricultural Research Institute-TARI)* ambae ndiyoTaasisi ya utafiti wa mbegu bora. Taasisi hii ikipatiwa fedha za kutosha ili kuzalisha mbegu bora ili kuboresha kilimo chenye tija.

#### 2.5.1.3. Mradi wa Maji wa Buzuruga

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea mradi wa maji uliopo katika eneo la Buzuruga jijini Mwanza ambao unachukua maji kutoka Ziwa Viktoria. Mradi huu ni chanzo cha pili cha uzalishaji na usambazaji wa maji katika jiji hilo na una uwezo wa kuzalisha maji lita **milioni 48** kwa siku. Mradi unatarajiwa kunufaisha wakazi 450,000 katika maeneo ya Nyamagana, Ilemela, Misungwi na Magu pindi utakapokamilika mwezi Oktoba, 2024. Jumla ya gharama ya mradi huu ni **Pauni milioni 31**.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo, Kamati iliishauri Serikali masuala yafuatayo: -

i. Kuhakikisha fedha za maendeleo zinatolewa kwa wakati ili kutekeleza miradi ya maendeleo;
ii. Kuhakikisha kunakuwa na umeme wa uhakika kwa ajili ya kuendesha mitambo ili kuepuka matumizi ya

umeme wa kangavuke (generator) ambao ni wa gharama;

iii. Wizara ya Maji ihakikishe kwamba kuna kuwa na miundombinu ya usambazaji ili maji yawafikie walengwa kikamilifu;
iv. Juhudi za kusambaza maji safi ziende sambamba na kuzuia uchafuzi wa Ziwa Viktoria ili wananchi wapate maji safi na salama;
v. Serikali ihakikishe dawa zinazotumika kutibu maji hazina madhara hasi kwa watumiaji; na
vi. Kudhibiti upotevu wa maji.

**2.5.1.4. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Kisasa ya Mwendokasi (SGR)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kV 220 kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya kisasa ya mwendokasi (SGR). Awamu ya kwanza ya mradi huu ambayo imekamilika kwa **asilimia 100,** uligharimu **shilingi bilioni 76.23.** Awamu hii ilihusisha upanuzi wa kituo cha Kinyerezi na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 kutoka Kinyerezi (Dar es Salaam) hadi Kingolwira (Morogoro). Njia hii ina urefu wa **Kilomita 160** ambayo itakuwa na umeme wa uhakika utakaolisha vituo vyote vinne vya kupoza umeme vilivyopo katika reli ya kisasa ya Pugu, Ruvu, Kidugalo na Kingolwira.

**Mheshimiwa Spika,** Awamu ya pili ya mradi wa njia ya kusafirisha umeme, umegawanyika katika lot mbili ya SGR Lot 2-1 na SGR Lot 2-2 inahusu ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 wenye urefu wa **kilomita 416** kutoka Msamvu-Morogoro hadi Kintiku-Singida. Gharama ya mradi ni **shilingi bilioni 97.5** na gharama ya mhandisi mshauri ambaye anasimamia kazi katika SGR Lot 2-1 na SGR Lot 2-2 ni **shilingi bilioni 4.53.** Zoezi la ulipaji wa fidia

kwa wananchi wanaopaswa kupisha maeneo ya ujenzi wa mradi linatekelezwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC). Katika sehemu ya awamu ya kwanza inayohusu ujenzi wa njia ya umeme kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, zoezi la ulipaji fidia limekamilika kwa **asilimia 100** ambapo jumla ya **shilingi bilioni 12.67** zililipwa kwa wananchi 4,792. Aidha, sehemu ya awamu ya pili zoezi la ulipaji wa fidia kutoka Msamvu (Morogoro) hadi Kintiku (Singida) limekamilika kwa **asilimia 100** ambapo jumla ya **shilingi bilioni 15.09** zimelipwa kwa wananchi 4,314.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa **asilimia 65** ya umeme utakaotumika katika uendeshaji wa treni ya kisasa unazalishwa na gesi ambayo inazalishwa na kusambazwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Kamati inashauri kwa kuwa visima vilivyopo ni vya muda mrefu kuna haja ya kufanya utafiti ili kupata visima vipya na kuongeza uzalishaji wa gesi ambao utachangia ongezeko la uzalishaji wa umeme.

#### 2.5.1.4.1. Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea Chuo Kikuu cha Mkwawa Iringa ambapo ujenzi wa mfumo mpya wa Manunuzi (Nest) unajengwa kwa lengo la kupewa mafunzo juu ya ujenzi wa mfumo huo. Kamati ilijulishwa kwamba mfumo huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kuokoa fedha za Serikali huku ukiendana na Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023. Aidha, mfumo huo utaongeza uwazi na uwajibikaji, kupunguza mianya ya rushwa na kuleta thamani halisi ya fedha katika manunuzi ya umma.

**2.5.1.4.2. Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Ofisi za Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro ili kuona utendaji kazi wa wakala katika kutekeleza majukumu yake. Kamati ilitembelea Mashamba ya Rijk Zwaan Mkoani Arusha na Mashamba ya Kahawa mkoani Kilimanjaro (Kilimanjaro Plantation) ili kujiridhisha endapo wakala anahakikisha waajiri wanazingatia masuala ya usalama kwa wafanyakazi na mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo Kamati ilishauri masuala yafuatayo**;**

- **i.** Wakala kupunguza gharama za kufanya vipimo vya afya kwa wafanyazi jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa na wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda kwa muda mrefu.
- **ii.** OSHA ilishauriwa kutembelea maeneo ya kazi na viwanda mara kwa mara ili kuhakikisha hakuna ukiukwaji wa Sheria za usalama mahala pa kazi**.**

**2.5.1.4.3. Utendaji kazi na miradi inayotekelezwa na Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea makao makuu ya Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania *(Tanzania Atomic Energy Commission-TAEC)* Mkoani Arusha. Lengo la ziara hiyo ilikuwa ni kukagua viwango vya tozo vinavyotozwa na Tume kama vina akisi huduma zinazotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa kwamba gharama zinazotozwa ni za chini ukilinganisha na huduma inayotolewa. Aidha,

Kamati ilitaarifiwa kwamba Tume imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo kuongeza matumizi ya TEHAMA katika ukaguzi wa sampuli mbalimbali. Hatua hii imesababisha Mataifa ya jirani kuja kupata uzoefu katika Tume hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Tume masuala yafutayo;

i. Kuandaa mtaala maalumu ili utumike katika kuanzisha Taasisi ya Umahiri ili kuzalisha wataalamu wengi zaidi nchini kuliko kuwapeleka kusoma nje ya nchi; na
ii. Kuweka mkakati maalumu wa kupata fedha ili kutoa misamaha kwa baadhi ya ada na tozo kwa wakulima wadogo ili waweze kuuza mazao yao nje ya nchi.

### 2.6. Mafunzo kwa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka mmoja Kamati ilipata mafunzo mbalimbali ili kuwajengea uwezo na kuwapatia ujuzi wajumbe wa Kamati katika kutekeleza majukumu yao. Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Wizara, Mamlaka, Wakala na Sekta Binafsi waliwezesha mafunzo kwa Kamati katika nyanja zifuatazo: -

i. Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE);
ii. Utendaji kazi wa mfumo wa Mahakama;
iii. Uendeshaji wa Mfuko wa Barabara pamoja na vyanzo vya mapato vya Mfuko wa huo;
iv. Mfumo wa Utekelezaji wa Miradi kwa njia ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)
v. Mifumo ya Kukusanya Mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya TANCIS, IDRAS na VAT-Refund;
vi. Sheria ya usalama na afya mahala pa kazi na changamoto zake (OSHA);
vii. Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma na Mfumo mpya wa Ununuzi wa NeST (PPRA);

viii. Uchambuzi wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na vipaumbele vyake;
ix. Kanuni za Usimamizi wa Biashara ya Hewa ukaa, kanuni za udhibiti na usimamizi na mchango wake katika Pato la Taifa;
x. Muundo na majukumu ya TRA;
xi. Mikakati ya Benki Kuu kutumia dhahabu kama akiba ya fedha za kigeni;
xii. Mafunzo kuhusu Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaoendeshwa na Kampuni ya TTCL;
xiii. Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja wa UTT AMIS;
xiv. Majukumu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)
xv. Ujenzi wa Barabara kwa Mfumo wa Engineering, Procurement, Construction- Financing (EPC+F);
xvi. Uhimilivu wa deni la Serikali pamoja na faida na hasara za kutumia mfumo wa EPC+F katika ujenzi wa barabara nchini;
xvii. Utendaji kazi wa Credit Reference Bureau, Mwenendo wa soko la Mitaji ya dhamana za Serikali baada ya Benki kuu ya Tanzania kushusha viwango vya riba;
xviii. Mizania ya Benki Kuu;
xix. Sekta ya mafuta na gesi;
xx. Mfumo wa uagizaji wa Mafuta wa Pamoja (Petroleum Bulk Procurement System) faida na hasara zake;
xxi. Udhibiti wa bei za Huduma za Nishati na Maji;
xxii. Usimamizi na usalama wa mifumo ya Serikali pamoja na utekelezaji wa sera ya Taifa ya TEHAMA;
xxiii. Namna ya kuchambua na kuzitumia Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali;
xxiv. Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);
xxv. Ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya barabara chini ya Wakala wa barabara vijijini na Mijini (TARURA); na
xxvi. Matokeo ya Sensa na Makazi na namna ya Kutumia Takwimu katika upangaji wa Mipango ya Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kushukuru Ofisi ya Bunge pamoja na Taasisi zote za Umma na Binafsi kwa kuipatia mafunzo

ambayo yameboresha utendaji kazi wake katika kufanya uchambuzi na kuishauri Serikali.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KATIKA KIPINDI CHA NUSU MWAKA (TAREHE 1 JULAI HADI TAREHE 31 DESEMBA 2023)

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali ililenga kufikia shabaha na malengo yafuatayo ya uchumi jumla na bajeti:

i. Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa **asilimia 5.2** mwaka 2023 kutoka ukuaji wa **asilimia 4.7** mwaka 2022;
ii. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa **asilimia 3.0 – 7.0** katika kipindi cha muda wa kati;

iii. Mapato ya kodi kufikia **asilimia 12.0** ya Pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/24 kutoka matarajio ya **asilimia 11.5** ya mwaka wa fedha 2022/23;
iv. Mapato ya ndani kufikia **asilimia 14.9** ya Pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/24 kutoka matarajio ya **asilimia 14.4** ya mwaka wa fedha 2022/23;
v. Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya **asilimia 3.0** ya Pato la Taifa; na
vi. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya Nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

**Mheshimiwa Spika,** hivyo, tathmini iliyofanywa na Kamati imezingatia shabaha na malengo kama yalivyobainishwa hapo juu.

## 3.1. VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA

### 3.1.1. Ukuaji wa Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa mwaka 2023 unatarajiwa kufikia **asilimia 5.2** ukilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 4.7** na **asilimia 4.9** kwa mwaka 2022 na 2021 mtawalia. Uchumi wa Taifa kwa kipindi cha miezi tisa ya mwaka 2023 ni wastani wa **asilimia 5.3**, hivyo kuna uwezekano wa kufikia ukuaji wa **asilimia 5.2**. kama ilivyo kwenye malengo na shabaha za Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa kiasi kikubwa unachangiwa na uwekezaji wa Serikali *(Public Sector Investment)* katika sekta za miundombinu, nishati, huduma za kijamii na usafirishaji. Jambo hili ni jema lakini linaashiria kwamba Sekta binafsi ambayo ndio injini ya kuendesha uchumi, haijaweza kushiriki ipasavyo katika uchocheaji wa ukuaji wa uchumi. Serikali ina jukumu la kuweka mazingira wezeshi ili Sekta Binafsi iyatumie kama fursa katika kuwekeza na kufanya biashara. Endapo Sekta binafsi haitaweza kutumia mazingira hayo ni wazi kwamba Serikali

haitapata manufaa ndani ya muda mfupi, wa kati na mrefu. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:

i. Kutekeleza miradi ya maendeleo yenye sura ya kibiashara kwa kushirikisha Sekta binafsi kwa mfumo wa Ubia baina ya Serikali na Sekta binafsi (PPP).
ii. Kuhakikisha mfumo na sera za kodi zinatabirika ili kuvutia wawekezaji; na
iii. Kutekeleza kikamilifu Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) ili kuchochea uwekezaji na kuondoa changamoto zilizopo.

### 3.1.2. Akiba ya Fedha za Kigeni

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwepo na changamoto ya uhaba wa fedha za kigeni hususan dola ya Marekani nchini, Serikali imeweza kuwa na akiba ya fedha za kigeni za kutosha. Hadi kufikia Desemba, 2023 akiba ya fedha za kigeni ilikuwa ni kiasi cha dola **za marekani bilioni 5.45** ikilinganishwa na **dola za marekani bilioni 5.18** katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la **asilimia 5.27.** Kiwango hiki kiliweza kukidhi uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa **miezi 4.5** ikiwa ni juu ya kiwango cha kimataifa cha **miezi 4.**

**Mheshimiwa Spika,** akiba hiyo inajumuisha akiba ya dhahabu fedha (gold reserve) yenye thamani ya **dola za marekani milioni 23** sawa na **kilo 354**. Hatua hii ni utekelezaji wa ushauri wa Kamati wa kuanza kutunza dhahabu kama sehemu ya akiba ya fedha za kigeni. Kwa kuwa dhahabu inanunuliwa kwa shilingi za kitanzania, hatua inawezesha kuongeza akiba ya fedha za kigeni kwa kutumia shilingi ya Tanzania.

### 3.1.3. Mfumuko wa Bei

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2023, mfumuko wa bei ulishuka hadi kufikia **asilimia 3.2** ukilinganishwa na **asilimia 4.8** katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kushuka kwa mfumuko wa bei kumechangiwa na kupungua kwa bei ya nafaka hususan

ngano, mchele, mahindi na mtama kufuatia hatua za Serikali kuongeza uzalishaji. Takwimu zinaonyesha kwamba utoshelevu wa chakula nchini ni **asilimia 124**, hivyo kusababisha mazao ya nafaka kupatikana kwa wingi na kwa bei nafuu. Aidha, mabadiliko ya Sheria ya Usalama wa Chakula Sura 249 ya mwaka 2023 yalilenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara ambayo yanaagizwa kwa wingi kutoka nje ya nchi. Jedwali Na 3 linaonyesha mwenendo wa uzalishaji katika kipindi cha nusu mwaka.

**Jedwali Na. 3. Uzalishaji wa Mazao ya Chakula Julai – Desemba, 2023**

| Aina | Nafaka | Yasiyonafaka | Jumla |
|---|---|---|---|
| Uzalishaji | 11,448,757 | 8,953,258 | 20,402,014 |
| Mahitaji | 10,427,327 | 5,963,077 | 16,390,404 |
| Uhaba(-)/ziada(+) | 1,021,430 | 2,990,181 | 4,011,161 |
| **Utoshelevu wa chakula (%)** | | | **124** |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo*

### 3.1.4. Mikopo Chechefu

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Novemba, 2023, mikopo chechefu ilipungua kufikia **asilimia 4.82** ikilinganishwa na **asilimia 7.17** katika kipindi kama hicho mwaka 2022, ikiwa ni chini ya ukomo wa wastani wa **asilimia 5.0**. Hatua hii ni ya kupongeza kwa kuwa inaashiria kwamba wakopaji wameweza kulipa mikopo yao kwa wakati. Ufanisi huu unaashiria kwamba sekta ya benki Nchini ni imara na inaweza kutoa mikopo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

### 3.1.5. Mikopo kwa Sekta Binafsi

**Mheshimiwa Spika,** mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa **asilimia 19.5** katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2023 ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 21.8** katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji wa mikopo

binafsi umeendelea kuwa juu ya makadirio ya ukuaji wa **asilimia 16.4** kwa mujibu wa Tamko la Sera ya Fedha Mwezi Juni 2023, kutokana na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha na kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** shughuli za kilimo zimeendelea kunufaika kwa kiwango kikubwa, ikifuatiwa na shughuli za ujenzi, uchimbaji madini na mawe pamoja na mikopo binafsi kama inavyoonekana katika jedwali na 2. Ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa shughuli za kilimo lilitokana pia na hatua za kisera zilizochukuliwa kwa lengo la kuchochea ukuaji wa mikopo kwa shughuli za kilimo kwa gharama nafuu ikiwemo kuanzishwa kwa mkopo maalumu wa **shilingi trilioni moja (1)** kutoka Benki Kuu. Hata hivyo, katika sekta ya kilimo kiasi kikubwa cha mikopo kilielekezwa kwenye biashara ya mazao ya kilimo na si katika uzalishaji.

**Jedwali Na. 4.Ukuaji wa Mikopo kwa Sekta Binafsi Julai – Novemba 2023 (%)**

| Shughuli/Mwezi | Julai | Agosti | Septemba | Oktoba | Novemba | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo | 46.4 | 52.4 | 55.5 | 34.6 | 38.9 | 45.6 |
| Usafiri na Mawasiliano | 22.2 | 11.0 | 15.0 | 14.3 | 25.3 | 17.6 |
| Majengo na Ujenzi | 26.1 | 30.5 | 22.6 | 37.3 | 23.3 | 28.0 |
| Binafsi | 20.1 | 19.4 | 20.7 | 20.5 | 20.4 | 20.2 |
| Madini na Mawe | 2.3 | 24.0 | 33.4 | 14.3 | 17.6 | 18.3 |
| Viwanda | 7.9 | 2.3 | -0.7 | 12.0 | 15.3 | 7.4 |
| Biashara | 18.7 | 22.9 | 20.0 | 7.1 | -0.4 | 13.6 |
| Hoteli na Migahawa | 1.4 | 1.6 | -3.3 | -4.2 | -0.9 | -1.1 |

***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi kuhusu dirisha la mkopo wa **shilingi trilioni 1** uliotolewa kupitia Tangazo la Benki Kuu la tarehe 27 Julai, 2021 na kubaini kwamba mpaka mwezi Desemba, 2023 kiasi cha mkopo kilichokuwa kimetolewa ni **shilingi bilioni 194.87** sawa na

**asilimia 19.49** ya **shilingi trilioni 1.** Hivyo, Kamati inashauri masuala yafuatayo: -

i. Kufanya tathmini ya matokeo ya mkopo huu kwenye sekta ya kilimo kuanzia Julai, 2021; na
ii. Kwa kuwa mkopo huu umeonyesha kuwa na mafanikio kwa upande wa sekta ya kilimo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kufufua mifuko ya dhamana (Guarantee Schemes) ili kuchochea ukuaji wa Sekta za Viwanda, Utalii, Mifugo na uvuvi.

### 3.1.6. Ujazi wa Fedha

**Mheshimiwa Spika,** ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M3) ulikua kwa wastani wa **asilimia 15.7** kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba, 2023. Ukuaji huu ni juu ya makadirio ya ukuaji wa **asilimia 10.1** kwa mujibu wa Tamko la Sera ya Fedha la Mwezi Juni 2023. Ukuaji huu ulitokana na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo huu umeonyesha kuvuka lengo lililokuwa limewekwa na Benki Kuu. Benki Kuu inaweka lengo la ukuaji wa ujazi wa fedha ili kufikia udhibiti wa bei na kuchochea ukuaji wa uchumi. Aidha, kutokana na ugumu wa kutambua kiasi cha fedha taslimu zilizopo kwenye mzunguko na kuongezeka kwa bidhaa mpya za huduma za kifedha na mifumo ya malipo, kumesababisha ugumu katika kuweka malengo yaliyo sahihi na kupanga maoteo ya ukuaji wa fedha unaoendana na mahitaji ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto hizi, Serikali kupitia Benki Kuu imeamua kubadili mfumo wa Sera ya Fedha na kuhamia kwenye mfumo unaotumia riba unaojulikana kama "*inflation targeting, interest rate au price-based monetary policy*". Benki Kuu itakuwa inatoa mwelekeo wa riba itakayotumika katika soko la fedha baina ya mabenki. Riba hiyo inajulikana kama Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate - CBR). Mabadiliko katika

riba hiyo yanaashiria mwelekeo wa Sera ya Fedha katika kuhakikisha kuwa ukwasi katika uchumi unaendana na malengo ya kudhibiti mfumuko wa bei na kuwezesha ukuaji wa uchumi. Riba hiyo pia itatumika kama kiashiria kimojawapo katika upangaji wa riba zinazotozwa na mabenki na taasisi nyingine za fedha nchini. Benki Kuu imeanza kutumia mfumo huu rasmi tarehe 19 Januari, 2024 kwa kuweka riba ya **asilimia 5.5** (CBR).

### 3.1.7. Thamani ya Shilingi

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2023, **dola moja ya Marekani** ilibadilishwa kwa wastani wa **shilingi 2,466.28** ikilinganishwa na **shilingi 2,318.33** katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na kushuka thamani kwa **asilimia 6.4**. Moja ya sababu zilizochangia kushuka kwa thamani ya shilingi ni ongezeko la bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nchi washirika wakuu wa kibiashara na kusababisha mahitaji makubwa ya fedha za kigeni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa ongezeko la mahitaji makubwa ya fedha za kigeni yamechangiwa pia na kiwango cha ubadilishaji wa fedha kisichoendana na hali halisi ya soko, ambapo viwango vya kubadilisha fedha vinavyotolewa na Benki Kuu haviendani na bei halisi ya soko. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya mfumo wa kupanga viwango vya ubadilishaji fedha ili viakisi hali halisi ya soko.

### 3.1.8. Mwenendo wa Viwango vya Riba

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba, 2023 wastani wa riba za mikopo ulikuwa **asilimia 15.54**, ikilinganishwa na **asilimia 16.10** katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, katika kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba, 2023 wastani wa riba za amana ulifikia **asilimia 7.06** ikilinganishwa na **asilimia 7.45** katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Mwenendo huu ulichagizwa na utekelezaji wa sera

wezeshi za kibajeti, usimamizi mzuri wa Sera ya Fedha katika kuchochea ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kupunguza riba za mikopo pamoja na kuongezeka kwa amana katika benki na hivyo kuongeza ukwasi katika sekta ya kibenki.

### 3.1.9. Thamani ya Bidhaa na Huduma

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2023, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma ilifikia **dola za Marekani bilioni 6.67** ikilinganishwa na **dola za Marekani bilioni 5.52** katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2023 ilipungua hadi kufikia **dola za Marekani bilioni 7.06** ikilinganishwa na **dola za Marekani bilioni 7.85** katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Takwimu zinaonyesha kwamba nakisi ya urari wa jumla wa bidhaa na huduma umepungua kutoka **dola za Marekani 2331.5** hadi **dola za Marekani 393.5** sawa na **asilimia 83.12**

**Mheshimiwa Spika,** ufanisi huu ulichangiwa na hatua zifuatazo;

i. Kuongeza uzalishaji wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kama mbolea, sukari, ngano na mafuta ya kupikia. Jitihada hizi zinapelekea kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni;
ii. Kuchagiza shughuli za uzalishaji wa bidhaa za kilimo na viwandani zinazozalishwa ndani ya nchi kwa lengo la kupunguza uagizaji wa bidhaa nje ya nchi (import substitution). Mfano, bidhaa za plastiki, ceramiki, mbolea, sukari na bidhaa nyingine;
iii. Kupungua kwa gharama za usafirishaji mizigo kutoka nje (freight charges) ikilinganishwa na kipindi cha mwaka 2022 na wakati wa janga la UVIKO-19;
iv. Kuongezeka kwa shughuli za utalii; na
v. Kupokelewa kwa misaada na mikopo yenye masharti nafuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua zake madhubuti katika kuhakikisha uchumi wetu unakuwa imara.

### 3.1.10. Deni la Serikali

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Desemba 2023, deni la Serikali lilikuwa **shilingi trilioni 87.47** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 74.75** katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la **asilimia 17.0**. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni **shilingi trilioni 56.79** na deni la ndani ni **shilingi trilioni 30.67**. Ongezeko la deni limetokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, elimu, afya, kilimo, mifugo, nishati na maji. Aidha, katika kipindi cha miezi 6 kuanzia Julai hadi Desemba, 2023 deni la Serikali limeongezeka kwa **shilingi trilioni 7.14** kutoka **shilingi trilioni 80.33** mwezi Juni, 2023 kufikia **shilingi trilioni 87.47** mwezi Desemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa deni la nje limeongezeka kutokana na mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha pamoja na riba kwa mikopo inayotegemea mabadiliko ya hali ya soko (floating rate). **Asilimia 28.3** ya deni la nje lipo kwenye riba inayobadilika kulingana na soko (flexible exchange rate) na **asilimia 71.7** ya deni ina riba isiyobadilika (fixed exchange rate). Kamati inashauri masuala yafuatayo: -

i. Kuimarisha makusanyo ya ndani na kuendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo – DCF ili kuondokana na mikopo ya kibiashara ambayo ina riba kubwa na inayobadilika kulingana na hali ya soko;
ii. Serikali ihakikishe Taasisi zake zinazojiendesha kibiashara zinalipa mikopo yake ili kuepuka kihatarishi cha Mikopo Sanjari; na

iii. Mikopo ya kibiashara ielekezwe katika miradi ambayo inaleta matokeo kwa muda mfupi.

**Jedwali Na. 5. Mgawanyo wa Deni la Serikali**

| Chanzo | Jumla (Bilioni) |
|---|---|
| **Deni la Nje** | **56,793.43** |
| Mikopo ya Kibiashara | 16,074.43 |
| Mikopo Nafuu | 40,719.00 |
| **Deni la Ndani** | **30,674.40** |
| Benki za Biashara | 8,289.68 |
| Taasisi za Fedha | 523.09 |
| Mifuko ya Jamii | 8,551.24 |
| Kampuni za Bima | 1,764.15 |
| Taasisi za Kigeni | 1,006.93 |
| Mashirika Madogo | 1,155.76 |
| Watu Binafsi | 2,245.22 |
| **Jumla ya Deni** | **87,467.83** |

***Chanzo**: Wizara ya Fedha*

**Jedwali Na.6. Tathmini ya Uhimilivu wa Deni (Asilimia)**

| Deni la nje | Ukomo | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uwiano wa Deni halisi kwa Pato la Taifa | 40 | 19 | 20.1 | 20.4 | 19.8 | 18.6 | 18.1 |
| Uwiano wa Deni halisi kwa Mauzo nje | 180 | 113.2 | 114.2 | 114.9 | 111.1 | 104.3 | 101.4 |
| Malipo ya deni kwa Mauzo nje | 15 | 12.7 | 11.1 | 11.5 | 11.2 | 12.2 | 11.3 |
| Uwiano wa Malipo ya deni kwa Mapato ya Serikali | 18 | 14.3 | 11.6 | 11.9 | 11.7 | 12.9 | 12 |
| **Deni la ndani na nje** | | | | | | | |
| Deni halisi kwa Pato la Taifa | 55 | 35.6 | 36.4 | 36.7 | 35.7 | 34.9 | 33.8 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni halisi kwa Mapato ya ndani ikijumuisha misaada | N/A | 232.9 | 209.2 | 207.3 | 204.2 | 200.7 | 194.7 |
| Malipo ya deni kwa Mapato ya ndani ikijumuisha misaada | N/A | 34.2 | 44.3 | 33.6 | 31.1 | 31.3 | 31.1 |

***Chanzo***: *Wizara ya Fedha*

### 3.2. Mwenendo wa Mapato na Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa kwa mwaka 2023/24 ni **shilingi trilioni 44.39**. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 30.31** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi trilioni 14.08** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi mwezi Desemba, 2023 Serikali ilikusanya jumla ya **shilingi trilioni 22.28** sawa na **asilimia 50.19** ya lengo la mwaka. Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Ukusanyaji huu wa mapato unaonyesha kwamba hadi kufika mwezi Juni, 2024 kuna uwezekano wa kukusanya mapato kati ya asilimia 90 hadi 98 ya lengo.

#### 3.2.1. Mwenendo wa Mapato hadi Desemba, 2023

##### 3.2.1.1. Mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2023 mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania ya kodi na yasiyo ya kodi yalifikia **shilingi trilioni 13.10** sawa na **asilimia 49.07** ya lengo la **shilingi trilioni 26.69.** Makusanyo hayo ni baada ya kulipa marejesho ya kodi ya **shilingi bilioni 570** sawa na **asilimia 51.55** ya lengo la mwaka la **shilingi trilioni 1.12.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kufikia ufanisi wa **asilimia 49.07** ya makusanyo ambayo ni kiashiria cha kuwa na sera za kodi madhubuti. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya marejesho ya kodi kwa wafanyabiashara pamoja na kuanzisha mfumo wa

kielektroniki wa *e-filing* kwa ajili ya kuwasilisha maombi ya marejesho ya kodi na misamaha ya faini na adhabu (penalty).

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko ya Kodi ambayo imezinduliwa rasmi tarehe 23 Januari, 2024. Hakika uanzishwaji wa Ofisi hii utasaidia kuondoa malalamiko ya walipa kodi na kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhamasisha wananchi kulipa kodi kwa hiari.

### 3.2.1.2. Mapato yasiyo ya Kodi

**Mheshimiwa Spika,** mapato yasiyo ya kodi yanajumuisha mapato ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali pamoja na michango na gawio la Mashirika, Mamlaka, Taasisi na Kampuni za Serikali. Hadi mwezi Desemba, 2023 mapato yasiyo ya kodi yalikuwa **shilingi trilioni 1.10** sawa na **asilimia 31.19.**

**Mheshimiwa Spika,** kutokufikia kwa lengo kumetokana na matumizi hafifu ya mifumo ya kukusanya mapato na kutokuwasilishwa kwa wakati kwa michango na gawio ya Mashirika na Taasisi za Serikali. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha Taasisi na Mashirika yanawasilisha michango na gawio kwa wakati kama sheria inavyoelekeza. Aidha, ihahikishe kuna matumizi sahihi ya mifumo ya kukusanya mapato na Taasisi zote za Serikali ziunganishwe katika mifumo hiyo.

**Jedwali Na. 7. Mchanganuo wa Mapato Yasiyo ya Kodi Julai Hadi Desemba, 2023 (shilingi milioni)**

| Fungu | Jina la Fungu | Makadirio 2023/24 | Halisi | Ufanisi % |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | 10,000.0 | 1,421.0 | 14.2 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 1,069,496.3 | 181,273.3 | 16.9 |
| 14 | Wizara ya Mambo ya Ndani - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji | 11,000.0 | 6,225.6 | 56.6 |
| 23 | Mhasibu Mkuu wa Serikali | 60,115.4 | 822.0 | 1.4 |
| 28 | Wizara ya Mambo ya Ndani - Jeshi la Polisi | 110,500.0 | 50,938.2 | 46.1 |
| 29 | Wizara ya Mambo ya Ndani- Jeshi la Magereza | 1,500.0 | 416.3 | 27.8 |
| 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa | 1,559.9 | 601.8 | 38.6 |
| 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu - Mpiga Chapa wa Serikali | 19,000.0 | 711.2 | 3.7 |
| 40 | Mfuko wa Mahakama | 12,571.2 | 5,283.8 | 42.0 |
| 43 | Wizara ya Kilimo | 6,677.3 | 3,535.9 | 53.0 |
| 45 | Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa | 900.0 | 184.9 | 20.5 |
| 46 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | 252,660.7 | 89,430.5 | 35.4 |
| 48 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 300,000.0 | 93,413.7 | 31.1 |
| 49 | Wizara ya Maji | 1,200.0 | 729.0 | 60.7 |
| | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi | 500.0 | 196.3 | 39.3 |
| 52 | Wizara ya Afya | 200,000.0 | 92,609.5 | 46.3 |
| 53 | Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalum | 8,500.0 | 2,754.8 | 32.4 |
| 64 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Uvuvi | 41,000.0 | 13,151.2 | 32.1 |
| 65 | Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu | 46,500.0 | 23,189.7 | 49.9 |
| 68 | Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 150,700.0 | 5,508.4 | 3.7 |
| 69 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 11,000.0 | 5,288.9 | 48.1 |
| 93 | Wizara ya Mambo ya Ndani -Idara ya Uhamiaji | 270,000.0 | 130,416.4 | 48.3 |
| 96 | Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo | 1,000.0 | 432.1 | 43.2 |
| 99 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Mifugo | 42,105.0 | 12,475.1 | 29.6 |
| 100 | Wizara ya Madini | 882,128.2 | 373,415.4 | 42.3 |
| | Wizara nyingine na Mikoa | 1,105.6 | 736.0 | 66.6 |
| | **Jumla** | **3,511,719.5** | **1,095,161.0** | 31.2 |

***Chanzo**: Wizara ya Fedha*

### 3.2.1.3. Mikopo na Misaada Nafuu

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Desemba 2023, **shilingi trilioni 4.03** zilipokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na **asilimia 73.73** ya makadirio ya **shilingi trilioni 5.47**. Ufanisi huu unatokana na kuimarika kwa diplomasia ya kiuchumi kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo kutokana na jitihada za **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika kufungua fursa za kiuchumi na kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo zinazofadhiliwa na fedha hizo ili kuendana na masharti ya wafadhili. Hatua hii itawezesha nchi kuendelea kupokea fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**Jedwali Na. 8. Mwenendo wa Mapato (Julai – Desemba, 2023) (shilingi bilioni)**

| Na | Chanzo | Bajeti (2023/24) | Utekelezaji (2023/24) | % |
|---|---|---|---|---|
| **A.** | **Mapato yanayokusanywa na TRA** | **26,691.20** | **13,096.80** | **49.07** |
| **B.** | **Mapato yasiyo ya kodi** | **3,511.70** | **1,095.20** | **31.19** |
| | Michango na Gawio ya Mashirika/Taasisi | 1,069.20 | 181.27 | 16.95 |
| | Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa | 2,442.20 | 913.89 | 37.42 |
| **C.** | **Jumla ya Mapato (A+B)** | **30,202.90** | **14,191.90** | **46.99** |
| **D.** | **Mapato ya Halmashauri** | **1,178.10** | 553.57 | 46.99 |
| **E.** | **Mikopo na Misaada ya Masharti Nafuu** | **5,466.21** | **4,030.35** | **73.73** |
| | Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 2,184.13 | 1,622.70 | 74.3 |
| | Misaada na Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta | 130.12 | 103.54 | 79.57 |

| Na | Chanzo | Bajeti (2023/24) | Utekelezaji (2023/24) | % |
|---|---|---|---|---|
| | Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo | 3,151.96 | 2,304.11 | 73.10 |
| **F.** | **Mikopo ya Nje yenye Masharti ya Kibiashara** | 2,100.5 | 747.2 | 35.57 |
| **G.** | **Malipo ya Mtaji** | 5,440.38 | 2,832.9 | 52.07 |
| | **Jumla ya Mapato** | **44,388.07** | **22,355.95** | **50.36** |

***Chanzo****: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Nusu Mwaka (Julai – Desemba, 2023)*

### 3.2.2. Mwenendo wa Matumizi hadi Desemba, 2023

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Desemba, 2023 Serikali ilikuwa imetumia jumla ya **shilingi trilioni 22.28** sawa na **asilimia 50.19** ya lengo la **shilingi trilioni 44.39.** Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida yalikuwa ni **shilingi trilioni 13.47** na matumizi ya maendeleo ni **shilingi trilioni 8.80.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa **asilimia 62** ya lengo la mwaka. Utolewaji huu wa fedha ni kiashiria kwamba Serikali imeendelea kuipa miradi ya maendeleo kipaumbele. Aidha, fedha nyingi zimeelekezwa kwenye miradi ya kimkakati na kukamilisha miradi mikubwa inayoendelea. Kamati inaamini pindi miradi hiyo itakapokamilika fedha nyingi zaidi zitaelekezwa kwenye miradi midogo. Vilevile, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuanza kutumia vyanzo bunifu kama vile hatifungani za buluu, hatifungani za kijani na hatifungani za miundombinu kama vilivyoainishwa katika mpango kugharamia bajeti yake ya maendeleo.

**Jedwali Na. 9. Mwenendo wa Matumizi (Julai – Desemba, 2023) (shilingi bilioni)**

| Na | Matumizi | Bajeti (2023/24) | Utekelezaji (2023/24) | Asilimia %ya bajeti |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **A.**Matumizi ya Kawaida | 30,310.8 | 13,473.5 | 44 |
| 2. | Mishahara | 10,882.1 | 4,941.0 | 45 |
| 3. | Deni la Serikali | 10,469.8 | 4,828.4 | 46 |
| 5. | Matumizi mengineyo | 8,959.0 | 3,704.1 | 41 |
| 6. | **B.**Matumizi ya Maendeleo | 14,077.2 | 8,805.8 | 62 |
| 7. | Fedha za Ndani | 10,795.1 | 7,356.0 | 68 |
| 8 | Fedha za nje | 3,282.1 | 1,449.8 | 44 |
| 9 | **Jumla (A+B)** | 44,388.00 | 22,279.30 | 50.19 |

***Chanzo**: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Nusu Mwaka (Julai – Desemba, 2023)*

### 3.3. Malimbikizo ya Madeni (Arrears)

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto inayoikabili usimamizi wa bajeti ya Serikali ni uwepo wa malimbikizo ya madeni ambayo hayajalipwa na kuendelea kuongezeka kila mwaka. Madeni haya yanajumuisha madeni ya watoa huduma, wakandarasi, malipo ya huduma za umeme na maji pamoja na madeni ya watumishi. Hadi kufikia Juni, 2022, Serikali ilikuwa na malimbikizo ya madeni ya **shilingi trilioni 3.23.** Kiambatisho Na A kinaonyesha mchanganuo wa umri wa madeni katika kipindi cha Juni, 2021.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwepo kwa Mpango Mkakati wa Kusimamia Malimbikizo ya Madeni wa mwaka 2018, bado kuna ongezeko la malimbikizo ya madeni. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa malimbikizo ya madeni yanatokana na sababu zifuatazo: -

i. Mapato kuwa chini ya matumizi katika kipindi husika ambayo yamekuwa chini ya maoteo ukilinganisha na matumizi;
ii. Baadhi ya Maafisa masuuli kutokuzingatia miongozo na sheria za usimamizi wa fedha za Serikali wakati wa kupanga bajeti wakati wa matumizi;
iii. Uhakiki wa madeni kuchukua muda mrefu ambapo hivi sasa huchukua takribani miezi 5 baada ya mwaka wa fedha kuisha;
iv. Matumizi hafifu ya mfumo wa FMIS kwa Taasisi za Serikali; na

v. Kutenga bajeti kwa shughuli zisizo za msingi na kuacha shughuli za msingi zinazozalisha madeni.

**Mheshimiwa Spika,** malimbikizo hay ya madeni yamekuwa na athari hasi sio tu kwa Serikali lakini pia kwa sekta binafsi na uchumi kwa ujumla. Athari hizo ni : -

i. Kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali kutokana na faini na adhabu zinazotokana na ucheleweshaji wa malipo;
ii. Wakandarasi na watoa huduma kuiuzia Serikali bidhaa na Huduma kwa bei ya juu ili kulinda thamani ya fedha kwa kuhofia Serikali kutokulipa kwa wakati;
iii. Ucheleweshaji na ukamilikaji wa miradi kutokana na ucheleweshaji wa malipo;
iv. Sekta binafsi kushindwa kuendelea kutoa huduma kwa Serikali kutokana na kutolipwa fedha zao;
v. Kupunguza kuaminika kwa Bajeti ya Serikali
vi. Kupungua kwa uwekezaji unaofanywa na Sekta binafsi; na
vii. Kuongezeka kwa madeni chechefu inayopelekea kuongezeka kwa gharama za mikopo kwa sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa ulipaji wa malimbikizo na Madeni ya Wazabuni wakandarasi na Watoa huduma. Hata hivyo, hivi sasa malimbikizo ya madeni ni zaidi ya **asilimia 12** ya matumizi yote ya Serikali ikiwa ni zaidi ya kiwango kinachokubalika kimataifa cha **asilimia 2** kwa miaka 3 mfululizo**.** Aidha, ucheleweshaji wa ulipaji wa madeni umekuwa na madhira kwa wadai. Mfano wengine kufilisiwa na wengine kufariki. Hivyo, ili Serikali iweze kupunguza malimbikizo ya madeni na kufikia kiwango stahiki, Kamati inashauri masuala yafuatayao:

i. Afisa masuuli kuhakikisha wanatenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni badala ya jukumu hili kufanywa na Serikali kuu pekee. Hatua hii italeta uwajibikaji na nidhamu katika upangaji bajeti;
ii. Afisa masuuli kutoingia mikataba mipya hadi kukamilika kwa malipo wa mikataba iliyopo;

iii. Taasisi za Serikali zinazodaiwa na Taasisi nyingine za Serikali kuhakikisha zinalipa madeni hayo ndani ya muda ikiwezekana wasitishiwe huduma hadi hapo watakapolipa madeni;

iv. Serikali kufanya tathmini ya madeni ya kila Taasisi zake na kuweka mkakati wa ulipaji kupitia bajeti za Taasisi husika; na

v. Mkakati wa ulipaji wa madeni uzingatie umri wa deni, faini na riba, amri ya mahakama na athari za kiuchumi na za kijamii.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa muda mfupi unaoweza kutumiwa na Serikali ni wa kukopa walau mara mbili ya kiwango kinachotengwa kila mwaka kulipa malimbikizo ya madeni cha Kati ya **shilingi bilioni 700 hadi 800.** Hivyo kwa kukopa mara mbili maana yake itapatikana **shilingi trilioni 1.4** hadi **trilioni 1.6** ili kulipa madeni ya muda mrefu na kupunguza malimbikizo ya riba. Malipo ya mkopo huo yatafanyika pole pole kulingana na makusanyo.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0. TATHIMINI YA UTEKELEZAJI WA MABORESHO YA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2023 PAMOJA NA MABADILIKO YA SHERIA YA USHURU WA FORODHA YA AFRIKA MASHARIKI YA MWAKA 2004

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilifanya maboresho katika mfumo wa ada, kodi, tozo na ushuru mbalimbali kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 ikiwa na dhamira ya kuendelea kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wa kutabirika. Maboresho haya yalilenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi hususani katika sekta za kimkakati ikijumuisha viwanda, kilimo, mifugo, uvuvi, miundombinu, biashara, uwekezaji, elimu pamoja na usafirishaji.

**Mheshimiwa Spika**, maboresho ya mfumo wa kodi yaliyofanywa kupitia Sheria ya fedha ya mwaka 2023 yanatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **shilingi bilioni 973.53** kwa mwaka wa fedha wa 2023/24. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka 2023/24, mapato halisi yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa hatua hizo yalifikia **shilingi bilioni 494.94** ikiwa ni ufanisi wa **asilimia 50.83** ya lengo la mwaka.

## 4.1. Tathmini ya Utekelezaji wa Baadhi ya Sheria zilizokuwa kwenye Sheria ya Fedha

**Mheshimiwa Spika**, tathmini ya utekelezaji wa baadhi ya Sheria umebaini kwamba kwa kiasi kikubwa Serikali imeweza kufikia lengo lililokuwa limekusudiwa kama ifuatavyo:-

### 4.1.1. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye malighafi za kutengeneza viautilifu vya mimea (insecticides) na vya mifugo (acaricides). Utekelezaji wa hatua hii ulitajariwa kupunguza mapato ya Serikali kwa **shilingi milioni 6.8** katika mwaka wa fedha 2023/24. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2023 mapato yalipungua kwa **shilingi milioni 3.2**. Hatua hii inaonyesha kwamba kuna muitikio chanya katika uagizaji wa malighafi za kutengeneza viuatilifu.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali pia ilisamehe kodi hii katika malighafi za kutengeneza hema za chuma (prefabricated structures) zitakazoagizwa na kutumiwa na wafugaji wa kuku. Hatua hii ilitarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 465.6** kwa mwaka 2023/24. Hadi Desemba, 2023 mapato ya Serikali yalipungua kwa **shilingi milioni 216.5** sawa na **asilimia 46.49**. Hatua hii inaashiria kwamba malengo ya kuchochea ufugaji wa kuku kisasa yamefikiwa.

### 4.1.2. Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82.

**Mheshimiwa Spika**, maboresho ya Sheria hii yalitarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi bilioni 58.89** kwa mwaka 2023/24. Hadi Desemba, 2023 mapato ya Serikali yalipungua kwa **shilingi bilioni 28.38** sawa na **asilimia 48.20** ya lengo la mwaka. Hatua hii ina maanisha kwamba Serikali imepunguza gharama za uendeshaji kwa Sekta binafsi pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini.

### 4.1.3. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332

**Mheshimiwa Spika,** moja ya marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria hii ni kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji kwa hisa zinazouzwa kwa lengo la kupata mtaji wa uendeshaji na si kuuza kampuni pale ambapo hisa zilizouzwa ni zaidi ya **asilimia 50**. Marekebisho hayo yalitarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi bilioni 21.13** katika mwaka wa fedha 2023/24. Hadi mwezi Desemba, Serikali imekusanya jumla ya **shilingi bilioni 6.89** sawa na **asilimia 32.59** ya lengo. Hatua hii inaonyesha kwamba imani ya wawekezaji imeongezeka na wananunua hisa za Kampuni za Kitanzania ili kuziongezea mtaji.

### 4.1.4. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilifanya marekebisho ya kutoza ushuru wa bidhaa wa **shilingi 20** kwa kilo moja ya saruji inayotoka nje ya nchi na inayozalishwa ndani ya nchi. Hatua hii ilitarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi bilioni 147.55**. Hadi mwezi Desemba 2023, Serikali ilikusanya **shilingi bilioni 42.13** sawa na **asilimia 28.55** ya lengo. Aidha, mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa ya saruji kutoka nje ya nchi kutoka kilo **milioni 15** hadi **kilo milioni 2,** ambao unachochea uzalishaji na matumizi ya saruji inayozalishwa nchini.

### 4.1.5. Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Sura ya 437

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilifanya marekebisho kwa kufuta tozo ya miamala kwenye miamala yote ya kielektroniki isipokuwa kwenye miamala ya kielektroniki ya kutoa fedha. Hatua hii ilitarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi bilioni 149.72** kwa mwaka 2023/24. Aidha, hadi Desemba 2023 marekebisho hayo yalipunguza mapato ya Serikali kwa **shilingi bilioni 42.89** sawa na **asilimia 28.65** ya lengo. Ufanisi huu umetokana na mifumo mingine ya ulipaji kama LIPA NAMBA na toa kwa tokeni kwa wakala ambayo inatumika zaidi na wananchi. Hivyo, kuna haja ya kuangalia upya uamuzi huu endapo umefikia malengo yaliyokusudiwa ya kuweka fedha kwenye mifumo rasmi kwa kuwa baadhi ya wananchi wanatumia mifumo mingine ya malipo kutoa fedha ili kukwepa tozo ya Serikali.

### 4.1.6. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilifanya marekebisho kwenye Sheria hii kwa kupunguza kodi ya mabango kutoka **shilingi 10,000** hadi **shilingi 7,000** na mabango yanayowaka ya matangazo (illuminated) kutoka **shilingi 13,000** hadi **shilingi 10,000**. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi bilioni 3.78** kwa mwaka 2023/24. Hadi Desemba, 2023 marekebisho hayo yalipunguza mapato ya Serikali kwa **shilingi milioni 743.6**, ikilinganishwa na matarajio ya kupungua kwa **shilingi bilioni 1.89** sawa na ufanisi wa **asilimia 39.36**. Hatua hii inaashiria kwamba kuna baadhi ya kodi zikipunguzwa zinaongeza ufanisi katika ukusanyaji wake.

### 4.1.7. Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004 (EAC Custom Management Act, 2004)

**Mheshimiwa Spika,** kupitia kikao cha Mawaziri wa fedha, uwekezaji, viwanda na biashara wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kilipendekeza kufanya maboresho kwenye

Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mapendekezo hayo yalilenga kuongeza kasi ya kufufua uchumi, kuhimili na kukabili athari za mabadiliko ya tabia nchi na kuimarisha sekta za uzalishaji. Hatua hii ilitarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 629.2**. Hadi kufikia Desemba, 2023 mapato ya Serikali yalipungua kwa shilingi **milioni 624.7** sawa na **asilimia 99.3** ya lengo. Mwenendo huu unaonyesha kuwa kiasi cha fedha kilichokusudiwa kupunguzwa kitazidi lengo lililokusudiwa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali pindi inapofanya maboresho kwenye mfumo wa Ushuru wa Forodha uchambuzi wa kina ufanyike ili kuhakikisha kwamba mapato ya Serikali hayaathiriwi zaidi ya kile kilichokusudiwa.

**4.2. Mapendekezo ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Sheria ya Fedha.**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupitia utekelezaji wa Sheria zote zilizoko kwenye Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 Kamati ina ushauri ufuatao:-

i. Serikali kuhakikisha kwamba kanuni za utekelezaji wa mabadiliko yanayopendekezwa zinaandaliwa sanjari na mapendekezo ya mabadiliko ili Bunge linaporidhia utekelezaji uende mara moja. Hivi sasa mabadiliko yanafanyika lakini utekelezaji wake huchelewa kuanza ili kusubiri kanuni zikamilike; na

ii. Muda mchache wa ushirikishwaji wadau wakati Kamati inachambua muswada wa Sheria ya Fedha na hivyo wadau wengi kushindwa kuwasilisha maoni na mapendekezo yao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuleta mapema Muswada huo Katika Kamati walau mwezi mmoja kabla ya kupitisha Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumpongeza **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kupokea mapendekezo ya Kamati na kuanzisha Kalenda ya Kodi kwa Kodi ya Ushuru wa bidhaa. Utaratibu unaotumika hivi sasa utakuwa unabadili viwango vya kodi za ushuru wa bidhaa

kila baada ya miaka mitatu. Utaratibu huu unakusudia kuleta uhimilivu wa bei kwa bidhaa na huduma zinazotozwa kodi hii na kuwa na Sera za kodi zinazotabirika.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0. MWELEKEO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA NA BAJETI YA SERIKALI HADI JUNI, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia tathmini ya mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla na utekelezaji wa bajeti ya Serikali, Kamati ina amini kwa kiasi kikubwa Serikali itafanikiwa kufikia malengo na shabaha iliyojiwekea. Kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla, Kamati inaushauri ufuatao: -

### 5.1. Malengo na Shabaha

i. Ukuaji wa Pato la Taifa unakadiriwa kufika **asilimia 5.2** katika mwaka 2023 ukizingatia kuwa katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka 2023, ukuaji ulifikia wastani wa **asilimia 5.3.** Hivyo, kuna uwezekano mkubwa kufikia malengo ya **asilimia 5.2.** Hata hivyo**,** kuna haja ya Serikali kutekeleza mikakati yake yenye lengo la kuhakikisha kwamba matarajio ya kushuka kwa ukuaji wa uchumi wa Dunia na kanda nyingine hauathiri ukuaji wa uchumi wa Taifa;

ii. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa tulivu na kubaki katika wigo wa **asilimia 3 hadi 7** ambao ni ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi na kikanda wa Jumuiya za Afrika Mashariki (EAC) na Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuchukua tahadhari na hatua madhubuti kufuatia mvua

zilizopitiliza kiasi zinazoendelea nchini zilizosababisha uharibifu wa mazao, miundombinu pamoja na mvurugiko wa mnyororo wa ugavi suala ambalo linaweza kusababisha upungufu wa chakula na hivyo kusababisha kuongeza kasi ya mfumuko wa bei.

**Jedwali Na.10. Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (Asilimia)**

| Nchi | 2022 | Matarajio | |
|---|---|---|---|
| | | 2023 | 2024 |
| Burundi | 18.9 | 20.1 | 16.1 |
| Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 9.3 | 19.1 | 10.6 |
| Kenya | 7.6 | 7.7 | 6.6 |
| Rwanda | 13.9 | 14.5 | 6 |
| Sudani ya Kusini | -3.2 | 16.3 | 13.6 |
| Tanzania | 4.4 | 4 | 4 |
| Uganda | 7.2 | 5.8 | 4.7 |
| **Wastani** | **8.3** | **12.5** | **8.8** |

**Chanzo**: *Wizara ya Fedha*

iii. Serikali kupitia Benki Kuu imeendelea kuboresha ufanisi wa utekelezaji wa Sera ya Fedha ambapo kuanzia Januari hadi Juni 2024, utekelezaji wa sera utaongozwa na mfumo mpya wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu katika kusimamia malengo mapana ya kiuchumi, kudhibiti mfumuko wa bei na kuchochea ukuaji wa uchumi. Kamati inashauri ili mfumo huu uweze kufanya kazi vizuri ni muhimu ukashirikisha sera nyingine za uchumi pamoja na kuwa na takwimu sahihi za viashiria vya uchumi.

iv. Serikali inashauriwa kuendelea kuchukua hatua madhubuti ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na akiba ya fedha za kigeni za kutosha ikiwa ni pamoja na kuendelea kutunza dhahabu fedha na kupunguza uagizaji wa bidhaa nje

zinazoweza kuzalishwa nchini (import substitution). Hatua hizi zitawezesha Taifa kuwa na akiba ya fedha iliyo imara na inayokidhi viwango vilivyowekwa vya miezi minne (4). Aidha, hatua hizi pia zitaimarisha thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine.

### 5.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Januari – Juni, 2024

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliweka malengo ya kukusanya mapato ya kodi ya Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) kufikia **asilimia 12.0** na mapato ya ndani kufikia **asilimia 14.9** ya Pato la Taifa kwa mwaka 2023. Malengo hayo yanatarajiwa kufikiwa kufuatia mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa mapato katika nusu ya kwanza Julai – Desemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia mwenendo huo, Kamati ina ushauri ufuatao: -

i. Kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato pamoja na kudhibiti matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo;
ii. Kusimamia matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato;
iii. Kuhakikisha Wizara, Idara na Taasisi zote nchini zinatumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato;
iv. Kuhakikisha mifumo yote nchini inasomana na kubadilishana taarifa;
v. Kuhakikisha kuwa gawio na michango stahiki inawasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa wakati; na
vi. Kuendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Corporation Framework-DCF) ili
vii. kupata mikopo na misaada yenye masharti nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina amini masuala yote haya yakitekelezwa Serikali itafikia malengo yake.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0. UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YALIYOTOKANA NA TAARIFA YA KAMATI YA MWAKA 2023

**Mheshimiwa Spika,** katika Taarifa ya Kamati ya mwaka 2023 kulikuwa na jumla ya mapendekezo 10 ambayo Bunge lako liliridhia yakawa maazimio ya Bunge. Maazimio hayo yalihusu: -

i. Serikali kuandaa Mpango wa Uhitaji wa Rasilimiali Watu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi ili taaluma zinazozalishwa katika vyuo vikuu na vya kati ziendane na maendeleo yetu ya uchumi na ndio iwe nyenzo kuu ya kugawanya fedha za mkopo wa Elimu ya Juu;
ii. Vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kupewa kipaumbele katika mradi wa Kujenga Kesho iliyo Bora (BBT) pamoja na ajira zinazotolewa na Kampuni Tanzu ya SUMA (JKT);
iii. Kuhuisha na kuunganisha mifumo ya TEHAMA ya kukusanyia mapato ili isomane kwa lengo la kupunguza upotevu wa mapato ya Serikali sambamba na kutoa kiasi cha **shilingi billioni 560** kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuboresha mifumo;
iv. Serikali kuchukua hatua kwa Wakurugenzi ambao wanashindwa kutenga Mkopo wa **asilimia 10** kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa Mujibu wa Sheria;
v. Kuongeza jumla ya **shilingi bilioni 170** kwa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ili fedha hizo zikaimarishe shughuli za uhifadhi na usimamizi;
vi. Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura (Contingency Fund) ili utumike kuhudumia mahitaji ya fedha za dharura bila kuathiri utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
vii. Serikali kuhakikisha kwamba uhamisho wa fedha unafuata Masharti ya Sheria ya Bajeti Sura 439 pamoja na Kanuni zake;
viii. Kutoa mtaji wa **shilingi bilioni 60** kwa Kampuni ya Mbolea *(Tanzania Fertiler Company-TFC)* ili iweze kununua mbolea moja kwa moja kwa wazalishaji wa mbolea;
ix. Kurejesha Tume ya Taifa ya Mipango *(National Planning Commission)*; na

x. Kuongeza jumla ya **shilingi bilioni 45.56** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya kipaumbele ya Sekta ya Anga.

### 6.1. Tathmini ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya tathmini ya utekelezaji wa maazimio yake na kubaini kwamba kati ya maazimio 10, Serikali imefanyia kazi maazimio 5 kikamilifu, inaendelea kufanyia kazi azimio 1 na maazimio 4 hayajafanyiwa kazi.

#### 6.1.1. Maazimio yaliyofanyiwa Kazi na Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kutekeleza kikamilifu maazimio yafuatayo:-

##### 6.1.1.1. Kurejesha Tume ya Taifa ya Mipango

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 2023 Serikali iliwasilisha Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango ya Taifa Sura ya 314 na ukapitishwa na Bunge na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais tarehe 14 Julai, 2023. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii na inatarajia Tume ikatekeleze majukumu yake kwa ufanisi na tija.

##### 6.1.1.2. Mtaji kwa Kampuni ya Taifa ya Mbolea – TFC

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali ilitoa mtaji wa jumla ya **shilingi bilioni 40** kwa Kampuni ya Mbolea (TFC) ukiwa ni pungufu ya **shilingi bilioni 20** ya kiasi kilichoazimiwa na Bunge cha **shilingi bilioni 60**. Mtaji huo umeiwezesha TFC kununua na kusambaza mbolea tani **25,000** (Urea tani 10,000 na DAP tani 15,000). Aidha, Serikali imeiwezesha Kampuni kupata mkopo wenye thamani ya **shilingi bilioni 70** (**US$ 27.364 Millioni)** kupitia Mradi wa Kuwezesha Upatikanaji wa pembejeo za Kilimo Tanzania (TAISP) utakaowezesha kununua mbolea tani **50,000**. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii, hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Kampuni hiyo bado haijaweza

kununua mbolea moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji kutokana na sababu mbalimbali.

**Mhesmiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada za Serikali kukamilisha mazungumzo na wazalishaji ili msimu unaofuata TFC iweze kununua mbolea moja kwa moja kwa wazalishaji bila kupitia kwa mawakala. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mapema iwezekanavyo hatua hizo za mazungumzo ili Kampuni hiyo iweze kununua mbolea moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji na kufanya mbolea inayouzwa na Kampuni hiyo ipatikane kwa bei nafuu.

#### 6.1.1.3. Mifumo ya TEHAMA ya kukusanya mapato kutosomana

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 Serikali ilitenga kiasi cha **shilingi bilioni 400** kwa ajili ya kuhuisha na kuhakikisha mifumo ya kukusanya mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inasomana. Kiasi hiki ni pungufu kwa **shilingi bilioni 160** ya kile kilichoazimiwa na Bunge cha **shilingi bilioni 560**. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 300** zilikuwa ni kwa ajili ya mifumo ya TEHAMA na **shilingi bilioni 100** ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** taasisi ambazo tayari mifumo yake ya TEHAMA imeunganishwa na ile ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa lengo la kubadilishana taarifa ni Mfumo wa GePG wa Wizara ya Fedha, Mfumo wa Mamlaka ya Bandari *(Terminal Operating System),* Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF),* Mfumo wa TAMISEMI wa Utoaji Leseni za Biashara *(TAUSI),* Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA),* Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF).*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii, hata hivyo, kabla ya kuanza kwa Mkutano wa 15 wa Bunge Kamati itatembelea Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kujiridhisha na utekelezaji wa kuhuisha mifumo kupitia fedha hizo.

#### 6.1.1.4. Usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia kwamba Serikali ihakikishe uhamisho wa fedha kati ya mafungu na ndani ya mafungu unafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na kanuni zake kufuatia ukiukwaji wa matakwa ya Sheria hiyo. Serikali imeahidi kuhakikisha kuwa uhamisho utakaofanywa ndani na baina ya mafungu unafuata kanuni, miongozo na sheria zilizopo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Serikali haijawasilisha *re-allocation warrant* ya mwaka wa fedha 2022/23, pindi itakapowasilishwa Kamati itafanya uchambuzi wa kina ili kubaini endapo masharti ya Sheria ya Bajeti Sura ya 439 yamezingatiwa au la.

#### 6.1.1.5. Mkopo wa asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia kwamba Halmshauri zote nchini kufuata utaratibu wa kisheria uliopo katika kutenga **asilimia 10** ya mkopo kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Aidha, hatua zichukuliwe kwa zile Halmashauri ambazo hazitatenga fedha hizo ikiwa imekusanya mapato. Serikali kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kukamilisha utaratibu mpya wa utoaji wa mikopo ya **asilimia 10**. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia na kuchukua hatua kwa Halmashauri ambazo hazitafikia lengo la kutoa mikopo kwa makundi mbalimbali.

### 6.1.2. Maazimio ambayo yapo katika hatua za utekelezaji

**Mheshimiwa Spika,** maazimio ambayo bado yanafanyiwa kazi ni yafuatayo: -

#### 6.1.2.1. Mpango wa Uhitaji wa Rasilimali watu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepokea Taarifa kwamba Serikali inaandaa Kiunzi cha Mpango wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma ambacho pamoja na mambo mengine, utekelezaji wake utafanyika kupitia Mkakati wa Mpango wa Rasilimali watu na Uendelezaji Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma, Mpango wa Rasilimali watu wa Miaka 10 na Mpango wa uendelezaji Rasilimali watu wa Miaka 10. Hivyo, Mkakati huo utaonesha ujuzi unaohitajika katika Utumishi wa Umma na hatimae Vyuo vitaweza kudahili kulingana na uhitaji husika. Hatua hiyo ya Serikali inafanyika sambamba na kutambua watumishi wa umma waliopo kwa kada na idadi ili kuwa na vigezo vya kitaalamu vya kubaini mahitaji halisi kwa kutumia mfumo wa *Human Resource Assessment*.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini iliyopendekezwa na Kamati ilikuwa ni Serikali kuandaa Mpango wa uhitaji kwa ajili ya Taifa zima na sio kwa watumishi wa umma pekee. Hivyo, mbali na hatua ambazo Serikali imeanza kuchukua, Kamati inaendelea kuitaka Serikali kufanya tathmini ya uhitaji wa rasilimali watu kwa Taifa zima kwa ajili ya maendeleo ya uchumi.

### 6.1.3. Maazimio ambayo hayajafanyiwa kazi

**Mheshimiwa Spika,** maazimio ambayo hayajafanyiwa kazi na Serikali ni yafuatayo: -

#### 6.1.3.1. Kuanzisha Mfuko wa Dharura (Contingecy Fund)

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia Serikali kuanzisha Mfuko wa Dharura ili Serikali iweze kukabiliana na dharura zitakazojitokeza ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Bajeti, Sura ya 439. Hata hivyo,

Serikali haijaweza kutekeleza azimio hili kutokana na utaratibu wa mfumo wetu wa kibajeti (cash budget).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaarifiwa kwamba Serikali imekuwa ikitumia utaratibu wa kawaida wa kutoa fedha ili kukabiliana na majanga mbalimbali ikiwemo ukame, magonjwa ya mlipuko na mafuriko mara yanapojitokeza.

**6.1.3.2. Nyongeza ya fedha kwa Shirika la Hifadhi la Taifa – TANAPA**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia TANAPA kuongezewa kiasi cha fedha **shilingi bilioni 170** katika bajeti ya mwaka 2023/2024 ili waweze kukidhi mahitaji ya msingi ya uhifadhi baada ya kuwa imeongezewa hifadhi. Hata hivyo, Serikali haijatekeleza azimio hili. Kutotekeleza azimio hili kunaweka Sekta ya Utalii mashakani.

**6.1.3.3. Kuongeza jumla ya shilingi bilioni 45.56 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya kipaumbele ya Sekta ya Anga**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikupokea Taarifa yoyote kuhusu utekelezaji wa azimio hili. Hivyo, ni wazi kwamba halijatekelezwa.

**6.1.3.4. Vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kupewa kipaumbele katika mradi wa Kujenga Kesho iliyo Bora (BBT) pamoja na ajira zinazotolewa na Kampuni Tanzu ya SUMA (JKT)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikupokea Taarifa yoyote kuhusu utekelezaji wa azimio hili. Hivyo, ni wazi kwamba halijatekelezwa.

## SEHEMU YA SABA

## 7.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA UJUMLA

### 7.1. Mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2023 sekta zilizokua kwa kasi ni pamoja na Sekta ya fedha na bima (**asilimia 16.0**), uchimbaji wa madini na mawe (**asilimia**

**10.2**), umeme (**asilimia 10.0**), huduma nyingine ikijumuisha sanaa na burudani (**asilimia 10.0**), malazi na chakula (**asilimia 8.9**) na habari na mawasiliano (**asilimia 7.9**). Na katika kipindi hicho sekta zilizokuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa ni pamoja na kilimo (**asilimia 24.8**), ujenzi (**asilimia 13.6**), uchimbaji wa madini na mawe (**asilimia 9.7**), biashara na matengenezo (**asilimia 8.4**), uchukuzi na uhifadhi wa mizigo (**asilimia 7.2**) na viwanda (**asilimia 6.9**). Sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa zina uhusiano wa moja kwa moja na uwekezaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya kilimo kwa muda mrefu imekuwa inaongoza kwenye uchangiaji wa Pato la Taifa. Hata hivyo, sekta hii sio miongoni mwa sekta zilizokua kwa kasi mbali na uwekezaji uliofanywa na Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo hadi kufikia **shilingi bilioni 970** katika mwaka wa fedha 2023/24. Kamati ina ushauri ufuatao:-

i. Wizara ya kilimo iendelee kufanya tathmini ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo na kubainisha ni maeneo yapi yanahitaji uwekezaji zaidi ili kuibua fursa fiche za sekta hii;
ii. Serikali ishirikiane na sekta binafsi katika kuongeza eneo la umwagiliaji ili kutimiza agenda ya 2030 ya kufikia hekta za umwagiliaji **milioni 8.5;**
iii. Serikali iendelee kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno ili kuongeza tija ya mazao na kunufaisha wakulima;
iv. Serikali kuendelea kuimarisha ushirikiano katika majukwaa ya Kimataifa ili kuzidi kufungua fursa za masoko pamoja na uwekezaji;
v. Kufanya mapinduzi ya kilimo kwa kuwekeza kwenye kilimo cha kisasa na chenye tija. Uwekezaji huu uende sambamba na elimu kwa wakulima; na
vi. Kuongeza thamani ya mazao yanayotokana na sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

## 7.2. Masoko ya Kikanda (Regional Integration)

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia mtikisiko wa kiuchumi inayoikabili dunia hususan katika nchi za washirika wakuu wa

biashara na Tanzania, kuna uwezekano ukaathiri biashara yetu na nchi husika. Hivyo, kuna haja ya Serikali kuimarisha mahusiano yake ya kikanda. Mtikisiko huu ni fursa ya kutafuta masoko mengine katika Kanda za SADC na EAC ili bidhaa zinazozalishwa nchini zisikose masoko.

### 7.3. Viwango vya Riba kwenye Mabenki kwa Watumishi wa Umma

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Juni, 2023 riba za mikopo zilikuwa **asilimia 16.04** ikiwa ni mara **3.5** ya mfumuko wa bei **(asilimia 4.6)**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba viwango hivi vya riba pamoja na ada na tozo kubwa kwenye miamala ndio chanzo cha faida kubwa kwa mabenki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri riba za mikopo kwa watumishi wa umma na waliopo kwenye ajira rasmi na za kimkataba zipunguzwe hadi kufika tarakimu moja kutokana na ukweli kwamba mikopo kwa watumishi wa umma inalipwa na waajiri moja kwa moja kutoka kwenye mishahara, na hivyo uwezekano wa kutolipika ni mdogo.

### 7.4. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kushiriki katika uwekezaji wa Hatifungani

**Mheshimiwa Spika,** Mifuko ya hifadhi ya jamii ni wanunuzi na wawekezaji wakubwa katika masoko ya mitaji nchini. Ushiriki wa mifuko hii unasaidia kuchangamsha soko na kuongeza mtaji kwenye Soko la Hisa la Dar-Es-Salaam (DSE). Kuanzia mwaka 2018 baada ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuunganishwa na kubakiwa na Mifuko ya Public Sector Social Security Fund – PSSSF na National Social Security Fund-NSSF ilipunguza ushiriki katika masoko ya mtaji. Kamati inaishauri Serikali kupitia mifuko hiyo kuongeza ushiriki kwenye masoko ya hisa ili kupanua wigo wa uwekezaji wa Mifuko hiyo pamoja na kuongeza thamani ya soko la Hisa la DSE.

**7.5. Utolewaji wa Fedha katika Mafungu Mbalimbali ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua utolewaji wa fedha katika mafungu mbalimbali na kubaini kwamba kuna tofauti kubwa kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na kilichotolewa. Mfano, kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa Wizara ya kilimo ni **shilingi bilioni 970.79** lakini kiasi cha fedha kilichotolewa hadi mwezi Desemba, 2023 ni **shilingi bilioni 311.45** sawa na **asilimia 33.45**. Aidha, fungu 05 (Tume ya Taifa ya Umwagiliaji) imepokea jumla ya **shilingi bilioni 67.46** kati ya **shilingi bilioni 373.51** zilizoidhinishwa na Bunge sawa na **asilimia 18**. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha hasa kwa sekta hizi za uzalishaji ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

## SEHEMU YA NANE

## 8.0. MAONI NA MAPENDEKEZO MAHUSUSI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati pamoja na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo: -

**8.1. Matumizi ya Seti ya Mitambo ya kuchimba visima na mabwawa**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali ilinunua na kusambaza seti 25 za mitambo ya kuchimba visima katika Mikoa 25, na seti 5 za mitambo ya ujenzi wa mabwawa katika kila kanda kwa gharama ya **shilingi bilioni 17.5**.

**NA KWA KUWA,** mitambo hiyo haitumiki kikamilifu hivi sasa kwa sababu baadhi ya Halmashauri zenye uwezo mdogo wa mapato haziwezi kukodi mitambo hiyo. Gharama za kuchimba kisima kimoja si chini ya **shilingi milioni 15.** Kukosekana kwa fedha katika baadhi ya Halmashauri kumesababisha mitambo hii isitumike kikamilifu.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali iweke utaratibu wa kutoa ruzuku kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ili kuziwezesha Halmashauri zisizokuwa na mapato ya kutosha zinufaike na mitambo hiyo. Vilevile, kuhakikisha Halmashauri zenye mapato ya kutosha na zenya uhitaji wa mitambo hiyo zinatenga Bajeti katika mwaka wa fedha 2024/25.

### 8.2. Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Fedha Haramu

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** mwaka 2006 Serikali ilianzisha Kitengo cha Kudhibiti Fedha haramu kupitia Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu (Financial Intelligence Unit – FIU) Sura ya 423 kwa madhumuni ya kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na wa silaha za maangamizi.

**NA KWA KUWA,** kitengo hiki kimekuwa kikikumbwa na changamoto mbalimbali kama vile ufinyu wa bajeti pamoja na uhaba wa watumishi ambapo watumishi wa kitengo hiki huazimwa toka taasisi mbalimbali Serikalini. Hali hii imekuwa ikisababisha kitengo hiki kupata ushirikiano hafifu kutoka kwa Mamlaka za udhibiti wa fedha haramu duniani kama vile *Egmont Group of Financial Intelligence Units, na The Financial Action Task Force* kutokana na hadhi yake.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali kubadilisha Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU) na kuwa Mamlaka ili ifanye kazi kwa kujitegemea kama ilivyo kwa nchi ya Zambia. Vilevile, Serikali ifanye mabadiliko kwenye Kifungu

cha 7 (1) na (3) cha Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423 ili kukiwezesha kitengo hiki kuwa na uwezo wa kuajiri na kuwajibisha watumishi kwa kuwa hivi sasa Kamishna wa Kitengo hiki hawezi kuwawajibisha.

**8.3. Utekelezaji wa miradi ya barabara kwa Mfumo wa Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mfumo wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ulianzishwa kwa lengo la kuisaidia Serikali kutekeleza miradi kwa njia ya ubia ili kupunguza utegemezi wa bajeti ya Serikali.

**NA KWA KUWA,** Mfuko wa Barabara umeelemewa na mahitaji ya ujenzi wa barabara ikilinganishwa na ukarabati wa barabara na madaraja, kutokana na kutegemea chanzo kikuu cha tozo cha **shilingi 263** kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli, na hivyo kusababisha uwezo wa Mfuko kuwa chini ya wastani wa **asilimia 50** ya mahitaji ya ujenzi na ukarabati wa barabara.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali itumie Mfumo wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi kujenga, barabara pamoja na madaraja. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia vyanzo mbadala kwa ajili ya kuongeza fedha kwenye Mfuko wa Barabara.

**8.4. Serikali iandae Sera na mkakati wa Ununuzi, Ugavi na uondoshaji Mali za Umma**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** pamoja na kwamba Bunge lilipitisha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023, hata hivyo Taifa halina Sera na Mkakati unaosimamia manunuzi katika Sekta ya Umma. Kukosekana kwa Sera na Mkakati kumesababisha Sheria ya Ununuzi wa Umma kufanyiwa mabadiliko mara sita tangu ilipotungwa kwa mara ya kwanza mwaka 2001.

**NA KWA KUWA,** inakadiriwa **asilimia 70** ya Bajeti yote ya Serikali hutumika kwa ajili ya Ununuzi wa Umma. Sera na

mkakati wa ununuzi wa umma utaiwezesha Serikali kutoa mwongozo, uratibu na uimara wa sekta nzima ya Ununuzi.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae Sera na Mkakati wa sekta ununuzi wa Umma.

### 8.5. Fedha za Mkopo wa ECF kujumuisha Sekta ya Utalii

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali ilipokea fedha za mkopo wenye thamani ya **dola ya Marekani bilioni 1.05** sawa na **shilingi trilioni 2.4** kupitia dirisha la Extended Credit Facility (ECF) kwa ajili ya kusaidia nchi masikini ambazo zina matatizo ya muda mrefu ya urari wa bidhaa na huduma, na mkopo huo umesaidia katika kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii zilizojitokeza kutokana na majanga yasiyo na udhibiti wa moja kwa moja wa Serikali. Mkopo huo ulitolewa kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi, Kilimo, wafanyabiashara wadogo, Nishati na Kaya maskini kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

**NA KWA KUWA,** Sekta ya Utalii imekua kwa kasi kutokana na juhudi za Mheshimiwa Rais kupitia Filamu ya *The Royal Tour* ambapo idadi ya watalii wa kimataifa iliongezeka kutoka wastani wa watalii **723,884** mwaka 2022 kufikia watali **864,402** mwaka 2023. Sekta hii ina mchango mkubwa katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni. Hata hivyo, Sekta hii bado inakabiliwa na changamoto ya miundombinu ya msingi kama vile barabara na viwanja vya ndege.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii kuwasilisha mahitaji ya fedha za maendeleo Wizara ya Fedha ili wapate mgao wa fedha za ECF mwaka ujao wa fedha 2024/25.

### 8.6. Uwepo wa Sera na Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA,** katika mwaka wa fedha 2022/23 ni miradi **253** tu ndio iliyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini kati ya takribani miradi **2,572** ikiwa ni sawa na **asilimia 9.84** ya miradi yote ya Serikali.

**NA KWA KUWA,** mwenendo huu umesababisha kuongezeka kwa gharama za miradi, miradi kutokukamilika kwa wakati, miradi kutekelezwa kwa muda mrefu kuliko ulivyokusudiwa, miradi kutokufikia malengo na miradi kutekelezwa chini ya kiwango. Haya ni matokeo ya kutokuwa na Sera pamoja na Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali kukamilisha utungaji wa Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini na kisha kutunga Sheria ambayo itabainisha mgawanyo wa majukumu na adhabu katika kufanya Ufuatiliji na Tathmini.

### 8.7. Kutungwa kwa Sheria na Sera ya Usimamizi wa Mali za Serikali (*Government Assets Management Division*)

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (*Government Assets Management Division*) inasimamia mali zote za Serikali zenye thamani ya **shilingi trilioni 77.5** kwa kutumia masharti ya kifungu cha 6A cha Sheria ya Fedha za Umma kinachompatia Mamlaka Katibu Mkuu HAZINA kusimamia mali zote za umma (*Oversight role over public assets*)

**NA KWA KUWA,** Idara hii haina Sheria na Sera mahsusi na hivyo kutegemea kifungu cha 6A cha Sheria ya Fedha za Umma, na hivyo kusababisha kukosekana kwa uwajibikaji, uwazi, udhibiti na ufanisi katika usimamizi wa mali za umma.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mali za Umma ili kuweka msingi wa kisheria utakaoongeza uwajibikaji, uwazi, udhibiti na ufanisi katika usimamizi wa mali za umma.

### 8.8. Riba za Mikopo katika Sekta ya Benki

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** riba za mikopo katika sekta ya benki zimeendelea kuwa juu kwa wastani wa **asilimia 16.04**

pamoja na hatua zote zilizochukuliwa na Benki Kuu za kupunguza sehemu ya Amana ambayo Benki za Biashara zinatakiwa kuweka Benki Kuu kwa mujibu wa Sheria (*Statutory Minimum Reserve – SMR)*, kutoa mkopo wa **shilingi trilioni 1** kupitia dirisha maalumu na kupunguza riba ya hati fungani za Serikali za muda mfupi na muda mrefu.

**NA KWA KUWA,** sekta ya benki nchini imeonekana inatengeneza faida kubwa kutokana na riba, ada na tozo mbalimbali. Uzoefu unaonyesha kwamba kiwango cha riba hakitarajiwi kuzidi mara 2 ya mfumuko wa bei. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba, 2023 wastani wa riba za mikopo ulikuwa **asilimia 15.54** huku mfumuko wa bei ukiwa ni **asilimia 3.6.**

**HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Benki Kuu ya Tanzania kufanya uchambuzi wa kina wa vigezo vinavyotumika na mabenki katika kupanga riba na kubainisha mikakati ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu ya kupunguza gharama hizo ili mikopo ipatikane kwa riba nafuu kwa ajili ya uwekezaji na ufanyaji biashara.

### 8.9. Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali imekuwa ikikusanya mapato yake kwa **asilimia 92.6, 98.2 na 98.5** kwa mwaka 2020/21, 2021/22 na 2022/23 mtawalia. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya ukosefu wa fedha kwa ajili ya kugharamia baadhi ya miradi ya maendeleo kutokana na kuongezeka kwa malimbikizo ya madeni ya watoa huduma, wakandarasi, malipo ya huduma za umeme na maji na madeni ya watumishi na hivyo kusababisha fedha zilizopo kutotosha kutekeleza miradi ya maendeleo ya mwaka husika.

**NA KWA KUWA,** hadi kufikia Juni, 2022 Serikali ilikuwa na malimbikizo ya madeni ya **shilingi trilioni 3.23,** ambayo ni zaidi ya **asilimia 12** ya matumizi yote ya Serikali ikiwa ni zaidi ya

kiwango kinachokubalika kimataifa cha **asilimia 2** kwa miaka 3 mfululizo**.**

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba ili fedha zipatikane kwa ajili ya miradi ya maendeleo Serikali kutekeleza yafuatayo;

i. Kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya mifumo ya kukusanya mapato na kuunganisha taasisi zote za Serikali katika mifumo hiyo;
ii. Kufanya mapitio ya matumizi ili kuondoa matumizi yasiyo na tija kwa Serikali; na
iii. Kupunguza misaada isiyo na tija ili kufikia **asilimia 1** ya lengo la Mpango; na
iv. Kuangalia uwezekano wa kufuta madeni ambayo Taasisi za Umma zinazodaiana kama hayasababishi hasara.

## SEHEMU YA TISA

## 9.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO

### 9.1. Mafanikio katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu, Kamati ilipata mafanikio yafuatayo: -

i. Kupokea, kujadili na kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria mbalimbali za kodi kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 iliyokuwa na jumla ya Sheria 18;
ii. Kurejeshwa kwa Sheria ya Mipango ya Kitaifa;
iii. Kutungwa upya kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023;
iv. Kufanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi;
v. Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi inayotokana na fedha za mkopo kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (Extended Credit Facility – ECF);
vi. Kusimamia utolewaji wa fedha na utekelezaji wa miradi kupitia mifuko iliyozingirwa (Ring Fenced Fund), Mfuko wa Maendeleo ya Reli, Mfuko wa Maendeleo ya Barabara, Mfuko wa Maji na Mfuko wa Maendeleo ya Umeme Vijijini;
vii. Kuwasilisha Bungeni jumla ya Taarifa nane. Taarifa hizo ni:-

a) Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya iliyokuwa Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka unaoishia 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/2024;
b) Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Mfuko wa Bunge, Mahakama na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT) kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mifuko hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024

c) Taarifa kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021, Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/24;
d) Taarifa kuhusu Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2023 (The Finance Bill, 2023);
e) Taarifa kuhusu Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Fedha Na. 13 wa mwaka 2023;
f) Taarifa kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2023/2024 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24;
g) Taarifa kuhusu Muswada wa Sheria ya Ubia baina Sekta ya Umma na Binafsi (PPP); na
h) Taarifa kuhusu Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma

viii. Kamati ilifanikiwa kupokea jumla ya Taarifa 64 ambapo ilizijadili na kuzichambua na kuzitolea mapendekezo mbalimbali;
ix. Kamati ilifanikiwa kukutana na Wizara za Serikali zaidi ya 15, Mamlaka zaidi ya 13, Taasisi zaidi ya 12 pamoja na Kampuni zaidi ya 4 za Serikali ili kupitia, kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri katika masuala mbalimbali; na
x. Kamati ilifanikiwa kukutana na wadau zaidi ya 33 kutoka Sekta binafsi na Taasisi za utafiti na kupokea na kujadili Maoni na Mapendekezo mbalimbali kuhusu masuala ya kodi na Sera za fedha.

## 9.2. Changamoto katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali, Kamati ilikabiliwa na changamoto zifuatazo: -

### 9.2.1. Ucheleweshwaji wa Taarifa kutoka Serikalini

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 136(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 Kamati ya Bajeti imejiwekea utaratibu kwamba Taarifa

zote ziwasilishwe kwenye Kamati siku tatu kabla ya siku ya kikao. Hata hivyo**,** baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali hazitekelezi sharti hilo. Hatua hii huathiri utendaji kazi wa Kamati kutokana na kukosa muda wa kutosha wa kuchambua taarifa ili kuweza kuishauri vizuri Serikali. Hivyo, Kamati inapendekeza Serikali kuzingatia utaratibu uliowekwa na Kamati wa kuwasilisha Taarifa ndani ya siku 3.

### 9.2.2. Tofauti ya Takwimu baina ya Wizara na Taasisi za Serikali kuhusiana na jambo moja

**Mheshimiwa Spika,** bado kumekuwa na changamoto ya utofauti wa takwimu baina ya Taasisi za Serikali kuhusiana na jambo moja. Utofauti huu umekuwa ukisababisha Kamati kushindwa kutoa ushauri sahihi. Mfano, kuna tofauti ya takwimu za ukusanyaji wa mapato ya Msajili wa Hazina zilizotolewa kwenye Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na Taarifa ya iliyowasilishwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Taarifa ya iliyowasilishwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina inaonyesha kwamba ofisi hii imekusanya jumla ya **shilingi bilioni 180.9.** Aidha, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali inaonyesha zimekusanywa jumla ya **Shilingi bilioni 181.3**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inaondoa utofauti wa takwimu zinazowasilishwa katika Kamati, ili kuondoa mkanganyiko katika uchambuzi wa taarifa hizo.

### 9.2.3. Kukosekana kwa utaratibu maalumu wa kikanuni wa kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Forodha wa Afrika Mashariki (East African Customs Management Act) ya mwaka 2004 hufanyika kupitia Bunge la Afrika Mashariki. Marekebisho hayo hufanyika baada ya kupokea mapendekezo kutoka nchi

wanachama. Hata hivyo, Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 hazijabainisha utaratibu rasmi kwa Waziri mwenye dhamana kuwasilisha mapendekezo ya Serikali Bungeni kabla ya kupitishwa na Bunge la Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Kanuni ya 136(8) Kamati imejiwekea utaratibu wa kukutana na Waziri wa Fedha na kujadili mapendekezo hayo kabla ya kuwasilishwa katika Bunge la Afrika Mashariki. Hivyo, Kamati inapendekeza kufanyika kwa mabadiliko ya Kanuni ili uwekwe utaratibu rasmi wa mapendekezo hayo kuwasilishwa kwenye Kamati kwa niaba ya Bunge. Hatua hii itahakikisha kwamba mapendekezo yanayowasilishwa katika Bunge la Afrika Mashariki yamezingatia maoni ya Bunge kwa maslahi mapana ya Taifa.

## SEHEMU YA KUMI

## 10.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mb Naibu Spika kwa miongozo yenu ambayo imeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi. Aidha, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mb Waziri wa Mipango na Uwekezaji na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mb Naibu Waziri wa Fedha kwa kushirikiana na Kamati katika kipindi chote cha vikao vya Kamati. Nawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha wakiongozwa na Dkt. Natu Mwamba Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Wataalamu kutoka Wizara ya Mipango na Uwekezaji wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Tausi Kida, pamoja na Wataalamu kutoka Tume ya Mipango wakiongozwa na Ndg. Lawrence Mafuru ambao walishirikiana na Kamati kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Mhe. Omari Kigua, Mb na Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango, maoni na ushauri wao ambao umesaidia Kamati kuisimamia Serikali ipasavyo. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifauatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe.Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Zainab Athumani Katimba, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe.Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe.Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe.Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe.Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** nimshukuru pia Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee Taarifa na Kamati na likubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

Daniel Baran Sillo, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

14 Februari, 2024

**KIAMBATISHO A. MALIMBIKIZO YA MADENI YA WAZABUNI WATOA HUDUMA NA WAKANDARASI JUNI 2021**

| Umri wa Malimbilkizo | Bidhaa na Huduma | Utilities | Pango la Ofisi | Ujenzi | Watumishi | Jumla ndogo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Chini ya siku 30** | 75,040,906,974 | 4,682,490,534 | 194,107,896 | 2,843,179,157 | 6,308,747,324 | **89,069,431,885** |
| **Zaidi ya siku 30 na Chini ya siku 60** | 328,127,821,082 | 7,290,199,116 | 1,329,983,096 | 65,166,240,991 | 16,267,995,655 | **418,182,239,939** |
| **Zaidi ya Siku 60 na Chini ya siku 90** | 635,604,468,049 | 11,153,398,550 | 6,263,725,237 | 252,773,789,186 | 23,361,336,785 | **929,156,717,807** |
| **Zaidi ya siku 90 na Chini ya siku 365** | 91,728,200,992 | 15,078,137,329 | 6,327,295,564 | 268,207,540,278 | 13,898,882,912 | **395,240,057,075** |
| **Zaidi ya siku 365 na Chini ya Miaka 2** | 456,617,062,847 | 27,331,115,472 | 69,699,951,629 | 426,842,445,782 | 80,215,716,685 | **1,060,706,292,416** |
| **Zaidi ya Miaka 2** | 712,721,845,298 | 17,807,306,431 | 21,203,670,648 | 264,898,772,882 | 178,573,104,969 | **1,195,204,700,228** |
| **Jumla Ndogo** | **2,299,840,305,243** | **83,342,647,432** | **105,018,734,069** | **1,280,731,968,276** | **318,625,784,329** | **4,087,559,439,349** |

**KIAMBATISHO B.**

**MALENGO NA MAKUSANYO HALISI KUTOKANA NA MAREKEBISHO YA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2023 KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI DISEMBA, 2023/24**

***Shilingi Milioni***

| Marekebisho ya Mfumo wa Kodi | Lengo la Mwaka | Lengo hadi Disemba | Makusanyo | Ufanisi (%) |
|---|---|---|---|---|
| Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148 | 70,015.5 | 35,007. 7 | 30,292. 2 | 86.6 |
| Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148 | 70,015. 5 | 35,007. 7 | 30,292. 2 | 86.5 |
| Kuongeza kima cha usajili kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani kinachotakiwa kwa mfanyabiashara kusajiliwa kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 200 | 75,333.1 | 37,666.5 | 34,276. 5 | 91.0 |
| Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye malighafi za kutengeneza viuatilifu vya mimea (insecticides) na vya mifugo (acaricides) zinazotambulika kwa HS Code 2916.32.00 (Benzalkonium Chloride) na HS Code 2916.32.00 (Glutaraldehyde) | -6.8 | -3.4 | -3.2 | 93.0 |
| Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye hema za chuma (prefabricated structures) zinazotambulika kwa HS Code 9406.20.90 zitakazoagizwa na kutumiwa na wafugaji wa kuku | -465.6 | -232.8 | -216.5 | 93.0 |
| Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Kiwango cha asilimia 0 kwenye bidhaa za mafuta ya kula yanayozalishwa nchini kwa mwaka mmoja | -4,845.2 | -2,422.6 | -3,764.7 | 155.4 |
| **Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332** | **138,692.1** | **69,346. 1** | **65,370. 2** | **94** |
| Kupunguza Kodi ya Ongezeko la Mtaji (Capital Gain Tax) kutoka asilimia 10 kwenye faida hadi Kodi ya Mapato ya 100 asilimia 3 ya thamani ya mauzo au | 21,130.0 | 10,565.0 | 6,885.9 | 65.2 |
| thamani ya ardhi iliyothaminishwa, (thamani yoyote kubwa | | | | |

| Marekebisho ya Mfumo wa Kodi | Lengo la Mwaka | Lengo hadi Disemba | Makusanyo | Ufanisi (%) |
|---|---|---|---|---|
| kati ya hizo) bila kujali gharama zilizowekezwa katika maeneo husika (investment costs) kwa walipakodi wasiotunza kumbukumbu za manunuzi au uendelezaji wa mali husika | | | | |
| kuweka utaratibu wa kukadiria kodi ya mapato kwa wasafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia viwango elekezi vya kodi kwa kila gari, kuanzia shilingi 250,000 mpaka 2,200,000 | 72,211.5 | 36,105.8 | 36,105. 8 | 100.0 |
| Kutoza Kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye malipo ya wachimbaji wadogo wa madini (Artisanal and small scale miners) | 44,712.4 | 22,356.2 | 832.9 | 3.7 |
| Kutoza Kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye malipo yatokanayo na uuzaji wa hewa ukaa (Verified Emmission Reduction) | 638.2 | 319.1 | 0.0 | 0.0 |
| **Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332** | **138,692.1** | **69,346. 1** | **65,370. 2** | **94** |
| Marekebisho ya viwango maalum vya ushuru (specific duty rates) kwa kiwango cha asilimia 10 ya bei kwenye bidhaa zisizo za petroli, na asilimia 20 ya bei kwenye bidhaa za bia na tumbaku | 299,662. 4 | 149,831. 2 | 149,38 1.7 | 99.7 |
| Kupunguza Ushuru wa Bidhaa kutoka shilingi 4,386 kwa lita hadi shilingi 2,466.45 kwa lita kwenye vinywaji vikali (Ready to Drink) vinavyozalishwa nchini | 779.1 | 389.6 | 439.4 | 112.8 |
| Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 20 kwa kila kilo moja ya Saruji inayotoka nje ya nchi na inayozalishwa ndani ya nchi | 147,549. 6 | 73,774.8 | 42,126. 0 | 57.1 |
| Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia 30 kwenye sigara na bidhaa za aina hiyo zinazotumia mbadala wa tumbaku zinazotambulika | 582.5 | 291.3 | 410.5 | 140.9 |
| kwa Hs code 2402.90.00; tumbaku inayovutwa kwa | | | | |

| Marekebisho ya Mfumo wa Kodi | Lengo la Mwaka | Lengo hadi Disemba | Makusanyo | Ufanisi (%) |
|---|---|---|---|---|
| kutumia bomba la maji inayotambulika kwa Hs code 2403.11.00; na sigara za kielektroniki, shisha na bidhaa za aina hiyo zinazotambulika kwa Hs codes 8543.40.10, 8543.40.90 na 9614.00.00 | | | | |
| Kutoza Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 20 kwenye mashine za Kamari (9504.30.00) zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na zinazozalishwa nchini | 1,365.4 | 682.7 | 514.2 | 75.3 |
| **Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004** | **-1,258.3** | **-629.2** | **-624.7** | **99.3** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha*

**KIAMBATISHO C.**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YATOKANAYO NA TAARIFA ZA MWAKA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI WA BUNGE**

| | HOJA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| **KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI** | | | | |
| **1.** | **Serikali iandae Mpango wa Uhitaji wa Rasilimali Watu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi.**<br><br>Serikali haina mpango wa Taifa unao onyesha mahitaji ya rasilimali watu kwa Taifa ambao ungekuwa nyenzo ya mgawo wa Mikopo ya Elimu ya Juu. | Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae Mpango wa Uhitaji wa Rasilimali watu ili taaluma zinazozalishwa katika vyuo vikuu na vya kati ziwe sawa na maendeleo yetu ya uchumi na ndio uwe nyenzo kuu ya kugawanya fedha za mkopo wa Elimu ya Juu. Hatua hii itasaidia kupunguza tatizo la ajira linalotokana na wahitimu kuwa na taaluma ambazo hazina soko. | | Serikali imepokea ushauri, kwa sasa inaandaa Kiunzi cha Mpango wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma ambacho pamoja na mambo mengine, utekelezaji wake utafanyika kupitia Mkakati wa Mpango wa Rasilimaliwatu na Uendelezaji Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma, Mpango wa Rasilimaliwatu wa Miaka 10 na Mpango wa uendelezaji Rasilimaliwatu wa Miaka 10.<br><br>Aidha, Mkakati wa Mpango wa Rasilimaliwatu na Uendelezaji Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma, utaandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya ujuzi ili kufikia malengo ya Mipango ya Maendeleo ya Taifa pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo. Hivyo, Mkakati huo utaonesha ujuzi unaohitajika katika Utumishi wa Umma na hatimae Vyuo vitaweza kudahili kulingana na uhitaji husika. |

| | HOJA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Hatua hiyo ya Serikali inafanyika Sambamba na kutambua watumishi wa umma waliopo kwa Kada na idadi ili kuwa na vigezo vya kitaalamu vya kubaini mahitaji halisi kwa kutumia mfumo wa Human Rasource Assessment. |
| **2.** | **Vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)**<br><br>Vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa JKT wapo wa aina 2. Wapo wanaojiunga kwa mujibu wa Sheria na wapo wanaojiunga kwa kujitolea. Changamoto kubwa iliyopo ni kukosekana kwa ajira mara baada ya kumaliza muda wao wa miaka mitatu hasa hawa ambao wako katika kundi la kujitolea. | Bunge linaazimia masuala yafuatayo: -<br><br>i) Kwanza ni kwa Wizara ya Kilimo kuanza na vijana ambao wako katika makambi mbalimbali ya jeshi kwa kujitolea;<br><br>ii) SUMA JKT wanapotangaza ajira za walinzi waanze kwanza na Vijana waliopo katika makambi ya jeshi wenye sifa stahiki ambao wanakaribia kumaliza mikataba na endapo hawatoshi ndipo watafutwe wengine. | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | |

| | HOJA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| **3.** | **Mifumo ya TEHAMA ya kukusanyia mapato kutosomana**<br><br>Bado kuna changamoto ya kutosomana kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka ya Mapato na Taasisi pamoja na Wizara kama vile TPA na Ofisi ya Rais Tamisemi. Kutosomana kwa mifumo kumesababisha kupotea kwa mapato ya Serikali na Ukaguzi wa Kodi (Tax Audit) kuwa mgumu. | Bunge linaazimia masuala yafuatayo;<br>i) Serikali kufanya uchambuzi wa mifumo yote ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato ili kuihuisha pamoja na kuiunganisha ili isomane. Hatua hii itapunguza upotevu wa mapato ya Serikali; na | Wizara ya Fedha | Mamlaka ya Mapato Tanzania imeendelea kulipa kipaumbele kikubwa suala la uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato. Katika uboreshaji huu, Mamlaka inatambua umuhimu mkubwa wa mifumo yake ya ndani (TIN, TANCIS, ITAX, EFDMS, E-Filling) kuwa na uwezo wa ubadilishanaji wa taarifa baina yake pamoja na mifumo ya nje ya Mamlaka. Baadhi ya Taasis ambazo tayari mifumo yake ya TEHAMA imeunganishwa na ile ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa lengo la kubadilishana taarifa ni pamoja na Mfumo wa GePG wa Wizara ya Fedha, Mfumo wa Mamlaka ya Bandari (Terminal Operating System), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Mfumo wa TAMISEMI wa Utoaji Leseni za Biashara (TAUSI), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). |
| | | ii) Serikali kutenga jumla ya **Shilingi billioni 560** kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili wahuishe mifumo yao na kuiunganisha kwa ajili ya | Wizara ya Fedha | Katika mwaka 2023/24, fedha zilizotengwa na Serikali kuwezesha usimikaji wa mifumo ya TEHAMA ya TRA ili iweze kusomana kwa lengo la kurahihisisha ulipaji kodi na kuondokana |

| | HOJA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | kukusanya mapato ya Serikali kikamilifu. | | na changamoto zinazojitokeza kwenye ulipaji Kodi ni kiasi cha shilingi bilioni 400 ambapo shilingi bilioni 300 ni kwa ajili ya mifumo ya TEHAMA na shilingi bilioni 100 ni Kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya TEHAMA.<br><br>Aidha, Serikali kupitia TRA inatekeleza mradi wa ujenzi wa mfumo wa usimamizi wa kodi za ndani uitwao IDRAS unaolenga kuunganisha shughuli zote za usimamizi wa kodi hizo badala ya kuwa na mifumo inayojitegemea na hivyo kuleta ugumu katika mawasiliano na mahusiano ya taarifa za mifumo hiyo. Mfumo wa IDRAS unatekelezwa kama sehemu ya Mpango Mkakati wa sita (6) wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ulioanza kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2022/23 na kutarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha 2026/27. |
| **4.** | **Mkopo wa Asilimia 10 kwa Wanawake, Vijana wa Watu Wenye Ulemavu**<br><br>Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 inaitaka kila Halmashauri kutenga | Bunge linaazimia Halmshauri zote kufuata utaratibu wa kisheria uliopo katika kutenga **asilimia 10** ya mkopo kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenyeulemavu. Aidha, hatua zichukuliwe kwa zile Halmashauri ambazo hazitafikia lengo hali ikiwa imekusanya mapato. | Ofisi ya Rais TAMISEMI | Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kukamilisha utaratibu Mpya wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10.<br><br>Kwa wakati huu Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe na Divisheni ya Maendeleo ya Jamii wanaendelea kutoa matibabu ya Afya ya akili na kuwajengea uwezo wa kujitambua na kuwapa elimu |

| | HOJA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.<br><br>**NA KWA KUWA,** suala hili ni takwa la kisheria Kamati imebaini kuwepo na masuala yafuatayo yanayokiuka sheria:<br><br>Kuna Halmashauri zimekuwa zikijumuisha marejesho ya mikopo kwenye asilimia 10 ya mikopo ya mwaka husika ili ama zionekane zimevuka lengo au zionekane zimefikia lengo tofauti na sheria inavyotaka; na<br><br>Halmashauri nyingine zimekuwa zinatoa chini ya kiwango cha asilimia 10 ya mapato ghafi, | | | ya Vikundi na ujasiriamali ili waweze kukidhi vigezo vya kupata mikopo ya asilimia 10.<br><br>Hata hivyo, mara baada ya utaratibu mpya wa mikopo ya asilimia 10 kutolewa Serikali itaendelea kusimamia na kuchukua hatua kwa Halmashauri ambazo hazitafikia lengo la kutoa mikopo kwa makundi mbalimbali. |

| | HOJA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | Mfano wa Halmashauri hizo ni Halmashauri ya Kibaha asilimia 3, Halmashauri za Wilaya ya Morogoro, Chato, Bukombe, Masasi na Nkasi zilichangia asilimia kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. | | | |
| | **Shirika la Hifadhi la Taifa - TANAPA Kuongezewa Hifadhi**<br><br>Mwaka 2019 Serikali iliongezea Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA) hifadhi mpya 6 na hivyo kufanya idadi za hifadhi zinazosimamiwa TANAPA kuwa 22. Vilevile, TANAPA iliongezewa Ofisi za Kanda 4, Vituo 5 vya Malikale na Ofisi Unganishi. Pamoja na | Bunge linaazimia TANAPA kuongezewa kiasi cha fedha Shilingi bilioni 170 katika bajeti ya mwaka 2023/2024 ili walau waweze kukidhi mahitaji ya msingi. Hatua hii sio tu itawezessha TANAPA kutekeleza shughuli zake lakini vilevile tunaunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia *Royal Tour* katika kuongeza utalii na kuvutia wawekezaji nchini katika sekta hiyo. | Wizara ya Fedha | Serikali inatambua umuhimu wa kugharamia shughuli za TANAPA katika utekelezaji wa dhana ya uhifadhi na utalii. Serikali imekuwa ikiiongezea TANAPA Bajeti mwaka hadi mwaka ambapo katika mwaka 2023/24 TANAPA iliidhinishiwa na Bunge bajeti ya shilingi **bilioni 504.9** ikilinganishwa na shilingi **bilioni 249.8** ya mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 102.2.<br><br>Aidha, Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya TANAPA ili kuchochea shughuli za utalii na kuvutia uwekezaji kadri ya uwezo wa Serikali utakavyoruhusu. |

| | HOJA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | ongezeko hilo la majukumu mapya bajeti ya uendeshaji ya Mamlaka ilibaki ile ile. | | | |
| **5.** | **Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura (Contigency Fund)**<br><br>Sheria ya Bajeti sura ya 439 katika vifungu vya 35, 36,37,38 na 39 inaelezea kuhusu umuhimu wa Serikali kuwa na mfuko wa dharura (Contigency fund) pamoja na utaratibu wa matumizi ya fedha katika Mfuko huo. | Bunge linaazimia kwamba Serikali ianzishe mfuko wa dharura na kutenga fedha kama sheria inavyoelekeza kwa ajili ya kukabiliana na dharura zitakazojitokeza. | Wizara ya Fedha | Serikali inatambua umuhimu wa uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Bajeti, Sura 439.<br><br>Aidha, kwa mujibu wa sheria hii Serikali inatakiwa kutenga asilimia moja (1%) ya bajeti ya Serikali ambapo fedha taslim inatakiwa kuwekwa kwenye akaunti maalum mpaka hapo dharura itakapojitokeza. Kulingana na mwenendo wa ukusanyaji wa mapato, kumekuwa na changamoto ya kufikia lengo la makusanyo ili kukidhi mahitaji, hali inayosababisha kushindwa kuanzishwa kwa Mfuko wa Dharura kulingana na takwa la sheria. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikitumia utaratibu wa kawaida wa kutoa fedha ili kukabiliana na majanga mbalimbali ikiwemo ukame, magonjwa ya mlipuko na mafuriko mara yanapojitokeza. |
| **6.** | **Usimamizi wa Mapato na Matumizi ya** | Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe uhamisho wa fedha kati ya | Wizara ya Fedha | Kifungu cha 41 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 pamoja na kanuni zake |

| | HOJA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | **Serikali**<br><br>Katika kipindi cha Julai hadi Juni 2022, Serikali ilikusanya jumla ya Shilingi trilioni 37.22 kutoka vyanzo vyote sawa na asilimia 97.2 ya bajeti nzima ya Serikali. | mafungu na ndani ya mafungu unafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti na kanuni zake. | | zinaelezea wigo wa kufanya uhamisho wa fedha ndani ya fungu (**within votes**) na kati ya mafungu (**between votes**).<br><br>**Uhamisho ndani ya fungu** (**within votes**) umefafanuliwa kwenye kanuni Na. 27(1) ya Sheria ya Bajeti Sura 439 inayo mruhusu Afisa wa Masuuli wa fungu kufanya uhamisho hadi kifikia ukomo wa **asilimia 7.** Aidha, kanuni Na. 27(3) imempa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kuruhusu kufanyika kwa uhamisho wa ndani ya fungu unaozidi **asilimia 7** na usiozidi **asimilia 10** ya bajeti ya fungu husika.<br><br>**Uhamisho baina ya mafungu** (**between votes**) unafafanuliwa kwenye kanuni Na. 28(2) ya Sheria ya Bajeti Sura 439 kama ilivyorekebishwa inayomtaka Waziri mwenye dhamna na masuala ya fedha kuruhusu kufanyika uhamisho usiozidi **asilimia 9** ya bajeti ya Serikali.<br><br>Kiwango cha ukomo wa uhamisho wa ndani ya Fungu kinakokotolewa kwa kulinganisha jumla ya uhamisho uliofanyika ndani ya Fungu ikijumuisha Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya maendeleo na Bajeti ya Fungu husika iliyoidhinishwa. |

| | HOJA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| **7.** | **Kuiwezesha Kampuni ya Taifa ya Mbolea (Tanzania Fertilizer Company – TFC)**<br><br>mahitaji ya mwaka ya mbole ni tani 698,260 mbolea ambayo inapatikana nchini kwa ajili ya matumizi ni tani 480,848 sawa na upungufu wa tani 217,412 hivyo kuna wakulima wengi wanakosa mbolea za kupandia na kukuzia kutokana na uhaba. Aidha, uzalishaji wa ndani wa mbolea ni asilimia 6 tu ya mahitaji yote. | Bunge linaazimia kwamba Serikali iiwezeshe Kampuni ya Taifa ya Mbolea (TFC) kwa mtaji wa **Shilingi bilioni 60** ili iweze kununua mbolea toka kwa wazalishaji moja kwa moja kuliko hali ilivyo sasa, ambapo Kampuni hii inalazimika kununua mbolea toka kwa mawakala. | Wizara ya Fedha | Serikali imeendelea kuiwezesha Kampuni ya Taifa ya Mbolea (TFC) kwa kuzingatia upatikanaji wa mapato. Aidha, kwa mwezi Oktoba 2023 jumla ya shilingi **bilioni 40** zimetolewa kwa ajili ya kuiwezesha TFC kununua mbolea moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji |
| **8.** | **Kurejesha Tume ya Taifa ya Mipango (Planning Commission)**<br><br>Tume ya Taifa ya Mipango katika nchi | Bunge linaazimia kwamba pamoja na dhamira ya Serikali ya kuirejesha Tume ya Taifa ya Mipango, Serikali irejesha Sheria ya Tume ya Mipango "Planning Commission Act (Cap 314)" kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 kama | Wizara ya Fedha | Serikali imetekeleza azimio hili kwa kuianzisha Tume ya Mipango kupitia Sheria ya Tume ya Mipango ya Mwaka 2023 chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. |

| | HOJA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | yoyote ndio chombo kikuu cha kupanga maendeleo na kuratibu masuala yote yanayohusu mipango ya nchi na uzoefu unaonesha ili Taifa lindelee ni lazima liwe na Tume ya Mipango. Mfano Mataifa ya Asia (Asian Tigers) yamefanikiwa kimaendeleo kwa kuwa na Tume za Mipango thabiti. | ilivyoondolewa kupitia Sheria hiyo ya Mwaka 2018 wakati ikiendelea na mchakato mwingine. | | |